# Nipashe

Jumatano Mei 27, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580242

The Guardian digital

www.ippmedia.com

nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710




## Wabunge sasa washinikiza bosi wa Nida atumbuliwe


UKURASA 2




UKURASA 11

# Serikali yamhoji Balozi Marekani

**NI** kuhusu utoaji wa taarifa zikiwamo za corona...*Endelea ukurasa 2*




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (wa pili kulia), akipokea mfano wa hundi ya dola milioni 100, kutoka kwa Mwakilishi Mkazi wa Kampuni ya Barrick, Hilaire Diarra (wa pili kushoto), jijini Dodoma jana, ikiwa ni sehemu ya malipo ya dola milioni 300, ambazo kampuni hiyo ilikubali kuilipa serikali kumaliza mzozo kati yao. Wengine ni Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Prof. Palamagamba Kabudi (kulia), Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo (wa tatu kulia) na Meneja wa Mgodi wa North Mara, Luiz Correia. **PICHA: WFM**

## BAA LA CORONA



Unapotumia vitakasa kusafisha mikono au sehemu unazofanyia kazi, hakikisha mchanganyiko wa vitakasa hivyo hauna sumu ya kudhuru mikono au sehemu unazofanyia kazi. WHO

* **Epuka mikusanyiko ya watu**
* **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
* **Epuka kusalimiana** kwa **kushikana mikono na kukumbatiana**
* **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## BARRICK YATOA BIL. 250/- MAKINIKIA

UKURASA 5

# Vyuo vyatoa masharti wanafunzi wanaporejea

UKURASA 2




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store



**MICHEZO** **MEXIME APONGEZA LIGI KUU KITUO KIMOJA** UK.23

**MAONI, KATUNI UK.6**

# Serikali yamhoji Balozi Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, imemwita Dk. Imni Patterson, Kaimu Balozi wa Marekani nchini, kwa lengo la kutoa ufafanuzi wa masuala mbalimbali ambayo ubalozi huo umekuwa ukiyaandika katika mitandao yake ya kijamii bila ya uthibitisho.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana jioni kwa vyombo vya habari na Emmanuel Buhohela, Mkurugenzi wa Kitengo cha Mawasiliano Serikali katika wizara hiyo, Kaimu Balozi huyo amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi Kanali Wilbert Ibuge, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo kwenye ofisi ndogo za wizara jijini Dar es Salaam.

Katika mazungumzo hayo, Katibu Mkuu alieleza masikitiko yake kutokana na namna ambavyo ubalozi huo umekuwa ukitoa taarifa mbalimbali za ushauri wa kiusafiri (travel advisory) zinazoandikwa na kusambazwa na Ubalozi wa Marekani kwenye mitandao ya kijamii.

Pia, taarifa zinazosambazwa na ubalozi huo kuhusu suala la namna Tanzania inavyoshughulikia ugonjwa wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona (Covid-19).

"Akitolea mfano, Katibu Mkuu amezitaja taarifa zilizotolewa na ubalozi huo siku ya Jumatano Mei 13, 2020 na ya siku ya Jumatatu Mei 25, 2020 kwenye mtandao wa Twitter wa ubalozi huo ambazo zote zilionekana kukusudiwa kutoa tahadhari kwa raia wa Marekani waliopo nchini na wanaotarajia kuja Tanzania kuwa Jiji la Dar es Salaam siyo salama kutokana na kuwapo idadi kubwa ya wagojwa wa Covid-19.

"Tahadhari hizo pia zimeendelea kudai kuwa hospitali nyingi jijini Dar es Salaam (bila ya kuzitaja hospitali hizo) zimefurika wagonjwa wa Covid-19, jambo ambalo siyo kweli na lina uwezekano wa kusababisha taharuki kwa Watanzania na wageni kutoka nje ya nchi ilhali hali halisi sivyo ndivyo inavyodaiwa," ilisomeka sehemu ya taarifa hiyo. Taarifa hiyo ilibainisha kuwa, Katibu Mkuu amemjulisha Kaimu Balozi kuhusu umuhimu wa ubalozi kutoa taarifa zilizothibitishwa hususan kwa sababu serikali haina kizuizi cha aina yoyote kwa mabalozi kutafuta na kupata taarifa sahihi na zenye ukweli.

Katika hatua nyingine, Katibu Mkuu amemshukuru Kaimu Balozi huyo kwa ushirikiano mzuri na wa kihistoria uliopo baina ya Tanzania na Marekani katika sekta mbalimbali ikiwamo afya, elimu, biashara, uwekezaji, ulinzi na usalama na maeneo mengine ya maendeleo.

# Wabunge washinikiza bosi Nida atumbuliwe

**Na Gwamaka Alipipi, DODOMA**

WABUNGE wameitaka serikali ichukue hatua dhidi ya Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (Nida) kutokana na dosari zilizoainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) katika mamlaka hiyo.

Miongoni mwa dosari kubwa katika utendaji wa Nida zilizoabainishwa na CAG, Charles Kichere, katika ripoti yake ya ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka wa fedha 2018/19, ni kushindwa kusimamia utoaji wa vitambulisho vya taifa kwa wananchi.

Wakichangia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu taarifa ya ukaguzi za CAG, wabunge walisema bungeni jijini hapa jana kuwa ukaguzi maalumu unapaswa kufanyika katika taasisi hiyo, ili kubaini kilichoko nyuma ya pazia.

Mbunge wa Nachingwea, Hassan Masala (CCM), alisema Mkurugenzi wa Nida anapaswa kuchukuliwa hatua kutokana na kushindwa kusimamia majukumu yake na kuisababishia hasara serikali.

"Ripoti ya CAG imebainisha maeneo yenye dosari katika utunzaji wa malighafi za kuzalisha vitambulisho vya taifa zenye thamani ya Sh. bilioni 42 na kutokuwapo kwa mikataba kati ya Nida na watumiaji wa taarifa za Nida, hivyo kuikosesha serikali mapato," alisema.

Masala aliongeza kuwa, kuna idadi kubwa ya Watanzania hadi leo hawana vitambulisho, na simu zao zimefungwa kutokana na uzembe wa Nida.

"Ni uzembe, Nida wameshindwa kutunza malighafi wakati wananchi wanakosa vitambulisho. Wametuingizia hasara kubwa, hivyo wachukuliwe hatua, wanashindwa kusimamia dhamana waliyokabidhiwa ya kutunza vifaa," alilalamika.

Balozi Adadi Rajabu, Mbunge wa Muheza (CCM), alisema Nida kushindwa kutunza malighafi zake na kuisabibishia hasara serikali ni kitendo cha aibu.

Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko (Chadema), alisema Watanzania waliopewa namba za vitambulisho ni milioni 27, lakini kati yao waliopewa vitambulisho ni milioni sita tu, idadi ambayo haivuki hata nusu ya walio na namba.



Matiko, mhadhiri wa zamani wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), alisema mamlaka zinazohusika, zinapaswa kufanya ukaguzi Nida, ili kubaini kinachosababisha kazi ya ugawaji vitambulisho kukwama.

Alisema mkurugenzi wa mamlaka hiyo anapaswa kuchukuliwa hatua pamoja na wote watakaobainika kuhusika katika kuihujumu taasisi hiyo.

"Kama 'project' (mradi) ya vitambulisho vya taifa imeshindikana, ifutwe turudi mfumo wa zamani wa kutumia vitambulisho vingine, kwa sababu Watanzania wanateseka," Matiko alishauri.

Maftaha Nachuma, Mbunge wa Mtwara Mjini (CUF), alisema: "Hivi sasa ninavyoongea, Nida wamefunga ofisi zao Mtwara Mjini, eti kwa sababu ya uwapo wa ugonjwa wa virusi vya corona, huu ni uzembe mkubwa."

Mbunge wa Jang'ombe, Ally Hassan King (CCM), alisema alijiandikisha mwaka 2014 kupata kitambulisho cha taifa, lakini hadi jana alikuwa hajafanikiwa kukipata.

"Tangu mwaka 2014, nimejiandikisha, tangu mwaka huo hadi leo (jana), ninapigwa danadana na sijapata kitambulisho. Kwa mujibu wa takwimu, Nida walitakiwa kutoa vitambulisho milioni 27, lakini hadi Aprili mwaka huu ni vitambulisho milioni sita tu walivyotoa," alisema.

Alisema kuna idadi kubwa ya Watanzania wambao wamesajili laini za simu kwa kutumia vitambulisho vya watu wengine. Alisema hayo yote yanafanyika kutokana na uzembe wa viongozi wa Nida ambao wanapaswa kuchukuliwa hatua.

Mbunge wa Bunda Vijijini, Boniphace Getere (CCM), alisema zaidi ya Sh. bilioni 42 zimetumiwa ovyo na Nida ambazo zingeweza kutumika kujenga zahanati 240 na vituo vya afya 80 nchini.

Getere alisema Mkurugenzi wa Nida anapaswa kuwajibishwa kwa kusababisha hasara hiyo pamoja na watendaji wengine ambao walihusika katika ubadhirifu huo.

**MAJIBU YA SERIKALI**

Akijibu hoja za wabunge, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene (pichani), alisema wameshaanza kuchukua hatua ya kuisafisha Nida kwa kuwaondoa watendaji walioku-wa wanasumbua.

Kuhusu Watanzania kutopata vitambulisho, Simbachawene alisema serikali imeshaagiza mitambo ya kutengenezea vitambulisho kutoka Ujerumani, ambayo imeshaingia nchini na kinachosubiriwa ni ufungwaji.

"Isingekuwa ugonjwa wa corona, wataalamu hao kutoka Ujerumani wangekuwa wameshakuja kufunga mtambo huo, lakini kwa sababu anga limeshafunguliwa hivyo watawasili muda wowote," alisema.

Simbachawene alisema mtambo huo utakuwa na uwezo wa kutoa vitambulisho 4,500 kwa saa, hivyo kuzalisha vitambulisho 144,000 ndani ya saa 16 na kwa miezi minne vitambulisho milioni 18.

Kuhusu mikataba, Simbachawene alisema Februari mwaka huu, Wizara ya Fedha, Wizara ya Mambo ya Ndani na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali waliruhusu Nida kuingia mikataba 63, na hadi sasa mikataba saba imeshatiwa saini, mikataba 14 ipo kwa wadau.

## Vyuo vyatoa tahadhari

**Na Romana Mallya**

VYUO mbalimbali vimetangaza masharti ya wanafunzi kurudi vyuoni ikiwa ni pamoja na kutoa ratiba ya masomo itakayopunguza uwapo wa idadi kubwa ya wanafunzi chuoni kwa wakati mmoja, ili kukabiliana na janga la corona.

Hatua hiyo imekuja ikiwa ni siku sita tangu Rais John Magufuli kutangaza kufungua vyuo vilivyokuwa vimefungwa kutokana na kuingia kwa baa la corona nchini Machi mwaka huu.

Kutokana na maelekezo hayo ya serikali, Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), kimewataka wanafunzi wake kukamilisha kulipa ada kwa mfumo wa malipo ya serikali na kujisajili kwa mfumo wa taarifa za wanafunzi (SIS) kuanzia tarehe ya tangazo lao walilolitoa.

"Mwisho wa usajili ni Juni 15, hakuna mwanafunzi atakayeruhusiwa kuingia chuoni baada ya hapo kama hajakamilisha usajili," lilisema tangazo hilo lilitotoka kwenye moja ya magazeti jana.

Pia, liliwataka wanafunzi kuangalia mikondo na ratiba za masomo kupitia SIS na kwenye tovuti ya chuo hicho.

Taarifa iliyotolewa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia Makamu Mkuu wake, ilibainisha kuwa wanafunzi wa kampasi zote wanapaswa kutambua kwamba masomo yataanza Juni Mosi.

"Wanafunzi wanaokaa mabweni ya chuo, wataanza kuingia kwenye vyumba vyao kama walivyokuwa wamepangiwa awali kuanzia Mei 30.

"Wanafunzi wanashauri kufika vyuoni kuanzia leo kwa ajili ya kufanya usajili na kukamilisha taratibu husika za kupokea fedha kwa wale wanufaika wa mikopo ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu," ilisema.

Pia, chuo kikuu hicho kikongwe zaidi nchini, kimewahimiza wanafunzi wote kuzingatia maelekezo yote ya serikali kuhusu udhibiti wa kuenea kwa virusi vya corona.

Vilevile, taarifa hiyo ilisema kuwa, ili kupunguza msongamano usio wa lazima, kwa mwanafunzi asiye na masomo siku husika, hataruhusiwa kuwapo eneo la chuo.

"Ratiba hizo zina mabadiliko ambayo yamelenga kupunguza uwapo wa wanafunzi wengi chuoni kwa wakati mmoja.

"Masomo yataanza Juni Mosi na wanafunzi wanaokaa hosteli za chuo wataruhusiwa kuingia chuoni Mei 31. Wanafunzi wachukue hatua ya kuvaa barakoa na kutumia vibukusi ili kujikinga na corona," iliagizwa kupitia taarifa hiyo.

## HABARI KITAIFA



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma (SACP), Gilles Muroto, akiwaonyesha waandishi wa habari jana sehemu ya magari 17, yanayodaiwa kuwa ya wizi yaliyokamatwa na jeshi hilo kwenye msako wa kutafuta wizi wa magari. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Polisi yakamata magari 17 ya wizi

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, limekamata magari 17 yanayodaiwa kuwa ya wizi yakiwa yamebadilishwa namba za usajili kufuatia msako mkali unaoendelea katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma.

Magari hayo yamekamatwa katika msako ulioanza Mei 19, hadi 22, mwaka huu kwa ushirikiano wa majeshi ya polisi mikoa mitano ambayo ni jirani na Jiji la Dodoma.

Kamanda wa Polisi mkoani hapa, Gilles Muroto, alisema magari hayo yamekutwa na makosa tofauti ikiwamo kutumia kadi za magari mengine yaliyopata ajali.

Vile vile, Kamanda Muroto alisema kuwa magari mengine wameyakata chassis kwa kufuta baadhi au kuongeza na kubadilisha baadhi ya namba au kubandika namba za usajili za magari mengine.

Alisema Jeshi la Polisi halitafumbia macho uhalifu huo ambao unachochea wizi wa magari nchini na kuongeza kuwa anayehusika atakamatwa na kuchukuliwa hatua kali za kisheria na magari yenye usajili wa bandia yatataifishwa.

Alisema magari yaliyokamatwa uchunguzi unaendelea na linamashikilia Helman Stephen aliyekamatwa akiwa na gari namba T. 891 BXY, Toyota Premio, ambalo lilikuwa linatumia kadi ya gari jingine.

Alisema gari namba T. 864 CQA Toyota IST mtuhumiwa akiwa ni Athumani Pambagu (29), mfanyabiashara na mkazi wa Nzuguni jijini Dodoma, na gari hiyo ikiwa chassis namba imekatwa na kuungwa na kibati kingine, pia vioo vimefutwa na kuandikwa namba nyingine.

Pia, gari namba T.661 CAV Land Cruiser Prado, kwenye kadi inasomeka Land Cruiser Corolado lenye chassis TTEBZ 991700033863 na namba hiyo pia imekamatwa kibati cha chassis kilichokatwa kinafanana na iliopo kwenye kadi.

Mtuhumiwa ni Mwami Monya (42), mfanyabiashara na mkazi wa Mpamaa Miyuji jijini Dodoma, gari namba T. 680 BWU aina ya Toyota Prado, lenye chassis namba, RZJI 200626277 na injini namba 3RZ3204070, inatumia usajili wa kadi, na faili la gari lingine huku mtuhumiwa akitajwa kuwa Ramadhan Mwita (42), mfanyabiashara na mkazi wa Kisasa, Dodoma.

Katika tukio jingine gari namba T. 237 DSJ aina ya Subaru likiwa Transit (IT), lilikuwa likisafirishwa kwenda Uganda, na dereva alipakia abiria wawili Misugusugu, Pwani ambao walikuwa wakienda Kahama, Shinyanga, lakini matokeo yake dereva alitishiwa silaha na kuporwa gari huku wakimwacha wamemfunga kamba na kutupwa porini eneo la Pandambili, Kongwa.

Alisema wamefanya ufuatiliaji kwa kushirikiana na wenzao wa Pwani na kufanikiwa kulikamata Kiwangwa, Bagamoyo Pwani, likiwa na namba bandia na watuhumiwa sita wamekamatwa.

Gari lingine ni T.642 APK aina ya RAV4 inatofautiana chassis na zilizopo kwenye kadi ya gari hilo, mtuhumiwa alitajwa kuwa ni Hosea Jonatham, mkazi wa Ndachi, Dodoma, nyingine ni yenye usajili T.743 DLT aina ya Raum, likiwa na kasoro katika usajili na bado linachunguzwa.

Jeshi hilo pia limemkamata Abdalah Mavumila akiwa na gari T.866 DFT aina ya Alphad, linatumia usajili wa kadi namba ya gari lingine, huku gari T.578 DBU Toyota Axio yenye chassis namba VZT240-5016540 injini namba INZ16540 na kubatizwa namba za gari lingine kwa kutumia nyaraka zisizo zake, mtuhumiwa ni Ally Abdallah (36).

Pia gari T.895 DSR Toyota IST lenye chassis namba NCP610028690 na injini namba INZA581375, mtuhumiwa akiwa Abdulahman Fuad (31), mfanyabiashara na mkazi wa Mlimwa C, jijini Dodoma.

Alisema gari namba T.926 Mitsubish Fuso lenye Chassis namba FH217C502904 mtuhumiwa ni Mwami Monya (42), mfanyabiashara na mkazi wa Mpamaa Miyuji Dodoma, gari lingine ni namba T.450 AST Scania lenye chassis namba Y5ZPE6X4Z01206603, mtuhumiwa Mwami Mwaluganje (42), mkazi wa Miyuji Dodoma.

Kadhalika gari T.870 CAM Toyota RAV4, lenye chassis namba 110148430 injini namba Z568DT, mtuhumiwa ni Yahya Bolingo (61), mfanyabiashara na mkazi Airport Dodoma, T.682 BMT Toyota RAV4 lenye chassis namba ZCA260051707 limebatizwa jina na kutumia nyaraka za gari lingine.

Mtuhumiwa mwingine ni Thomas Tesha, akiwa na gari T.992BAK aina ya Fuso, huku Bakari Omary akiwa na gari T.383 CXF aina ya Fuso na gari lingine ambalo limekamatwa lina namba T.380 AGP Toyota Chaser lililotelekezwa.

# Nyati azua taharuki kijijini, wananchi waji 'lockdown'

**Na Gurian Adolf, NKASI**

WAKAZI wa kijiji cha Kate, kata ya Kate wilayani Nkasi, mkoani Rukwa, wameingia katika taharuki baada ya nyati kuvamia kijiji hicho na kusababisha wananchi kujifungia ndani na kushindwa kwenda kwenye shughuli zao ikiwamo mashambani.

Akizungumzia tukio hilo, Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Philbert Kwimba, alisema nyati huyo alianza kuonekana tangu juzi kijijini hapo na kusababisha wananchi kushindwa kutoka nje ya makazi yao wakihofia usalama wao na kujikuta wakishindwa kwenda shamba kuendelea na shughuli za mavuno.

Ofisa Tarafa wa Kate, Bazilio Mazungwa, alisema nyati huyo amekutwa nyumbani kwa mfugaji mmoja kijijini hapo juzi, majira ya saa moja asubuhi na kufanya wananchi washindwe kutoka nje ya makazi yao kwa kuogopa kukutana naye.

Alisema kufuatia hali hiyo, wametoa taarifa kwenye mamlaka husika ya serikali ya wilaya kuomba msaada ili wananchi wa kijiji hicho waweze kuendelea na shughuli zao za kawaida ikiwa ni pamoja na kuwaepusha na madhara yanayoweza kutokea.

Alisema hadi sasa hakuna taarifa zozote mbaya zilizoripotiwa tangu nyati huyo alipovamia kijiji hicho na wananchi wameendelea kuchukua tahadhari kujiepusha naye.

Kaimu Ofisa Maliasili na Utalii wa Wilaya ya Nkasi, Frank Wakungwa, alisema idara yake kwa kushirikiana na askari wa wanyamapori (TAWA) wamekwenda eneo la tukio kukabiliana na nyati huyo ili kuondoa hofu inayowakabili wakazi wa kijiji hicho ambacho mpaka sasa wakazi wake hawana amani kutokana na uwapo wake.

Alidai kuwa kuna namna mbili ya kufanya, kwanza ni kumrejesha nyati huyo ndani ya hifadhi ya Lwafwi alikotokea au kumuua kama ataonekana kuwa ni hatarishi na kazi ya kumsaka bado inaendelea.




**Bonite Bottlers Ltd** inayo furaha kuwaletea **Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa wa LITA 6, LITA 12 na LITA 18.9.** Tumewekeza katika mitambo ya kisasa ya kuzalisha maji katika ujazo mkubwa ili kuwawezesha wateja, wanywaji na wadau wetu kupata maji kwa ajili ya matumizi ya majumbani, maofisini na kwenye taasisi mbalimbali.

**UPATIKANAJI:-**

- Maji ya Kilimanjaro katika ujazo mkubwa yanapatikana kwenye depoti zetu zote zilizoko mikoani, maduka na wauzaji wa jumla nchi nzima.
- Kwa Wateja wetu wa Mkoa wa Dar es Salaam, unaweza kununua maji ya kunywa ya Kilimanjaro ukiwa nyumbani kwa njia ya mtandao kupitia makampuni ya usambazaji bidhaa tunayoshirikiana nayo ambayo ni **Shoponline Tanzania www.shoponline.co.tz** na Piki Deliveries **www.piki.co.tz** .

Ni matumaini yetu mtaendelea kutuunga mkono kwa kuburudika na maji kutoka kilele cha Afrika.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI:**

**Moshi:** +255 755851170 au +255 27 2754422/7, **Arusha:** +255 756339532 au +255 27 2544876, **Dar:** +255 754635988 au +255 22 700450/655, **Morogoro:** +255 782546090, **Dodoma:** +255 787495439, **Karatu:** +255 757673123, **Babati:** +255 765459199, **Singida:** +255 755271963, **Tanga:** +255 763407979, **Mbeya:** +255 757266235, **Mwanza:** +255 742099191, **Nzega:** +255 746031412

**MAJI YA KUNYWA YA KILIMANJARO NI MAJI YA KUAMINIKA KILA SIKU!**

MAKALA MAALUM

# Taasisi Ustawi Jamii inavyosaidia korti kesi mirathi, wazazi kugombania watoto

**Na Enock Charles**

TAASISI ya Ustawi wa Jamii ni Taasisi ya Serikali chini ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto iliyoanzishwa kwa dhumuni la kutoa mafunzo kwa Watanzania watakaoihudumia jamii katika kada ya ustawi wa jamii na kuboresha hali za maisha ya wananchi.

Mkuu wa Taasisi hiyo, Dk. Joyce Nyoni, anasema katika miaka mitano ya serikali ya awamu ya tano, taasisi imeendelea kutekeleza dhima yake ya kutoa mafunzo katika kozi za ustawi wa jamii, menejimenti ya rasilimali watu, uhusiano kazini na menejimeti ya umma, uongozi wa biashara, sheria, uamuzi na usuluhishi, kufanya utafiti na kutoa ushauri weledi katika maeneo ya ustawi wa jamii ambayo ni muhimu katika ujenzi wa uchumi imara wa taifa.

Anasema kwamba, mpaka sasa taasisi inajivunia huduma wanazotoa maofisa ustawi wa jamii katika jamii na inawatia moyo ambao kwa namna ya pekee wanatoa huduma katika kipindi kipindi hiki ambacho dunia inakabiliwa na baa la virusi vya corona vinavyosababisha homa kali ya mapafu (Covid-19).

Dk. Joyce anasema taasisi inaendelea kuwa chachu ya maendeleo na mafanikio ya serikali katika kuboresha maisha na hali ya jamii ya Watanzania kwa kutoa huduma mbalimbali ambazo ni pamoja na kuwa na programu za kwenda kutoa ushauri kwa jamii na kuboresha mafunzo kwa wanafunzi inaowapika.

"Kwa mfano, taasisi imeendesha mafunzo ya muda mfupi ya malezi ya watoto ambayo yameendeshwa na wahadhiri wabobezi wa masuala ya watoto kwa makundi ya kinamama na walezi katika vituo vya kulea watoto.

"Mafunzo hayo yalilenga katika kuwajengea uwezo wazazi na walezi kufahamu mabadiliko ya kiteknolojia ambayo yanaathiri tabia na makuzi, namna ya kuweka uwiano sawa wa kulea watoto katika ukinzani wa utandawazi na maadili ya Kitanzania, mila na desturi zetu.

"Mafunzo haya pia yamewapa wazazi na walezi ujuzi wa kuwapatia watoto lishe bora, utambuzi wa mazingira anayokulia mtoto na athari zake, mabadiliko ya kitabia ya mtoto, jinsi ya kuadhibu mtoto, mbinu za kutambua na kuzuia misongo ya mawazo ya wazazi isiwaathiri watoto.

"Haya ni baadhi ya mambo katika elimu pana ya malezi na makuzi ya mtoto ambayo taasisi imetoa kwa jamii na inaendelea kutoa ili kuona haki, ubora wa maisha na malezi ya watoto yanaimarika Tanzania na kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la watoto wa mitaani na kuona pia watoto walio katika vituo vya kulelea watoto, wanapata malezi bora," anafafanua.

Dk. Nyoni anabainisha kuwa, mwaka huu taasisi imeanza kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu bila malipo kwa wananchi kwenye masuala mbalimbali kama vile ushauri wa kisheria juu ya wajibu wa malezi ya watoto, elimu ya haki na wajibu wa wazazi katika malezi ya watoto mwenye ulemavu, elimu ya ulinzi wa mtoto kwa mujibu wa sheria, elimu na unasihi wa uhusiano wa ndoa, kutembelea shule za sekondari na kutoa elimu dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya na ushauri wa maendeleo ya taaluma za wanafunzi za baadaye.



Jengo la utawala la Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

Anasema kuwa katika maeneo haya, taasisi inaisaidia serikali kupunguza kesi nyingi katika mahakama za wazazi kugombania watoto, wanandoa kuwa katika mitafaruku ya kugawana mali baada ya kuachana, watoto kupata manyanyaso katika familia wanazoishi, kuondoa ukatili wa watoto wa namna zote kwa kutoa elimu kwa jamii nzima na hasa walezi wa watoto na wanandoa.

"Tarehe 14 hadi 17 Machi mwaka huu, Taasisi ya Ustawi wa Jamii ilitoa huduma tajwa kwa jamii inayozunguka taasisi na pia ilialika wananchi na makundi mbalimbali kupitia matangazo ya mitandao na redio kufika katika taasisi kupata huduma hizi ambazo zilihudhuriwa kwa wingi na elimu iliyotolewa na wanufaisha wengi waliofika, walipata ufumbuzi wa matatizo waliokuwa nayo, mengi yakiwa ya kifamilia.

"Kwa upande wa uraibu wa dawa za kulevya na athari zake, taasisi inaisaidia serikali; kwanza, kwa kutoa ushauri nasaha kwa vijana walio katika hatari ya kupotoka na ushawishi wa makundi rika kujihusisha na matumizi ya dawa za kulevya na matendo mengine mengi kinyume cha sheria na utamaduni wetu.

"Hili tumelifanya kwa wanafunzi wa shule za sekondari za Manzese na Salma Kikwete, Kijitonyama jijini Dar es Salaam ambazo tumeanza nazo kutoa elimu katika programu yetu endelevu hii ya kutoa elimu kwa jamii," anasema.

Anabainisha kuwa wanafunzi walifundshwa jinsi ya kujitambua na kutambua wajibu na mchango wao kama vijana na jinsi utegemezi wa nguvu kazi yao kwa taifa unavyohitajika, huku wakifundishwa mbinu za kukabili vishawishi vya kuingia katika matumizi ya dawa za kulevya.

Mkuu wa Idara ya Ustawi wa Jamii Taaluma, Dk. William Manyama, anasema wahadhiri waliobobea kwenye ushauri nasaha wa uraibu pia walifika katika kituo cha kutoa dawa kwa waathirika wa uraibu wa dawa za kulevya katika Hospitali ya Mwananyamala na kutoa elimu kuhusu namna wanavyoweza kurudi tena kwenye jamii na kukubalika kama watu waadilifu wanaoweza kupewa ushirikiano kwenye ajira, kukopeshwa mitaji ya kufanya biashara na kurudi kuwa nguvu kazi ya taifa.

"Hii itasaidia watu walio katika harakati za kuondokana na uraibu kujikubali, kujiamini na kurudi na kuwa mabalozi wazuri wa kupinga matumizi ya dawa za kulevya na zaidi kusaidia mamlaka kutokomeza biashara hii haramu," anasema.

Katika kuhakikisha wanafunzi wanaongeza ubunifu na weledi, Dk. Nyoni anasema taasisi imeshaanzisha programu ya kuwatafutia na kusimamia mazoezi kazini kwa vitendo ambayo yatadumu kwa muda wa miezi 12, ambayo mwanafunzi baada ya kuhitimu, atapata nafasi ya kufanya kazi katika ofisi mbalimbali za wadau wa kada ya ustawi wa jamii.

Anasema wameanzishwa utaratibu huo ili kuondoa ombwe lililoko kati ya mbinu na uwezo wa mhitimu katika kazi na mahitaji ya soko la ajira.

"Programu hii itawajengea uwezo mkubwa wanafunzi kuelewa taratibu za kazi, mbinu za kutatua matatizo kutekeleza kazi zao, pia kumjengea ujasiri mhitimu huyu ambaye anatarajiwa kutoka mchango mkubwa katika ofisi yake husika, na mwisho programu hii itatazimiwa kuzalisha wahitimu wengi ambao watakuwa na uwezo wa kuanzisha ofisi zao wenyewe na kujiajiri na hata kuajiri wenzao hapo baadaye.

"Taasisi pia imeanzisha kituo cha ubunifu chuoni Kijitonyama ambacho kinawawezesha wanafunzi kuwasilisha mawazo yao ya kiubunifu kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii na kuweza kuona ni njinsi gani wanatumia teknolojia iliyopo kwa ufumbuzi wa matatizo mbalimbali katika jamii yetu ya kitanzania.

"Kituo hiki kinawaleta pamoja wadau mbalimbali ili kubadilishana uzoefu baina ya wanafunzi wa taasisi pamoja na wabunifu kutoka ndani na nje ya nchi na kutengeneza ubunifu wao.

"Tunaendelea kuboresha utoaji wa elimu ya jamii nchini na kuongeza wigo wa upatikanaji wa elimu hiyo, tanatarajia pia kuimarisha Kampasi ya Kisangara, Mwanga ambayo sasa imekuwa sehemu ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii katika kutoa mafunzo nchini," alisema.


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED

Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent& Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADAWA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA (BOA)** tutauza kwa mnada wa hadhara dhamana ya mdaiwa tajwa hapo chini ,mahali dhamana ilipo kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini ;Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | **COSMAS & BLANDINA INVESTMENT** | Nyumba ya makazi yenye kiwanja na.67, Kitalu "**C**"Ardhi na.167943 Iliyopo maeneo ya Chanika,iliyopo kwa jina la **COSMAS LAURENT KAMANGU** | 13/6/2020 |

MASHART YA MNADA

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.

Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugezi Mtendaji
Bank of Africa
Head Office,
NDC Development House,
ohio street-kivukoni
P.O. BOX 3054,
DAR ES SALAAM
Tel: +255-22-2110104/2111290
Fax: +255-22-2113740

157504

## HABARI KITAIFA

# Barrick yakabidhi serikali bil. 250/-

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imepokea dola za Marekani milioni 100 (sawa na Sh. bilioni 250), zilizotolewa na kampuni ya Barrick ikiwa ni fidia kwa Tanzania kutokana na kampuni hiyo kuchimba na kusafirisha madini bila serikali kupata kiwango sahihi.

Akizungumza jana wakati wa hafla fupi ya kupokea hundi hiyo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, alisema fedha hizo ni malipo ya awali ya Dola za Marekani milioni 300 (sawa na kiasi cha shilingi bilioni 750).

Aidha, alisema pande husika zimekubaliana mpango wa malipo wa bakaa ya kiasi cha Dola za Marekani milioni 200.

Aidha, aliishukuru kampuni hiyo kwa kuonyesha dhamira ya dhati ya ushirikiano mzuri kwenye mwelekeo mpya wa sekta ya madini Tanzania, ambao umekubalika na pande zote kwa manufaa ya pande zote husika.

Kwa mujibu wa Waziri Mpango, mbali ya makubaliano hayo, kampuni ya Barrick imekubali kutoa kiasi cha Dola za Marekani milioni 5 kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa mtambo wa kuchaka madini nchini (smelter).

Pia, kuanzisha ushirikiano na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na kutoa hadi Dola za Marekani milioni 10 kwa kipindi cha miaka 10 kwa ajili ya utoaji wa mafunzo yanayohusu sekta ya madini.

Mengine ni kutoa hadi Dola za Marekani 6 kwa kila 'ounce' ya madini itakayouzwa (ikijumuisha mchango kwenye Mfuko wa Maendeleo ulioanzishwa na Kampuni ya Barrick Tanzania) ili kusaidia jamii zinazozunguka maeneo ya migodi.

Pia, kutoa kiasi cha Dola za Marekani milioni 40 kwa ajili ya kuboresha kipande cha barabara kati ya Bulyanhulu na Mwanza na kujenga nyumba na miundombinu yake.

"Tunatumaini kwamba pande zote mbili zinazohusika katika makubaliano zitaheshimu makubaliano na kuhakikisha yanatekelezwa. Nawahakikishia kwamba serikali imedhamiria kwa dhati kutekeleza makubaliano hayo," alibainisha.

Waziri Mpango alisema uthibitisho wa hilo ni hivi karibuni serikali kuruhusu makontena na makinikia ya madini 277.

"Serikali imedhamiria kwa dhati kuwa ushirikiano wenye usawa katika sekta ya madini utasaidia kuleta fedha ambazo zitasaidia katika kuboresha maisha ya Watanzania," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Mpango, masuala muhimu yaliyokubalika ni kuunda Shirika la Madini la Twiga lenye umiliki wa pamoja lililoanzishwa Oktoba 20, mwaka jana, litakalofanya kazi nchini katika kusimamia uendeshaji wa migodi ya Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara pamoja na migodi mingine nchini, ambapo serikali ya Tanzania itashiriki katika utoaji wa maamuzi kuhusu uendeshaji wa migodi, mipango, manunuzi pamoja na masoko ya madini.

Alibainisha faida za kiuchumi zitokanazo na migodi ya Bulyanhulu, Buzwagi na North Mara zigawanywe kwa msingi wa usawa kati ya washirika yaani 50/50 ambapo hisa za serikali zinazotokana na faida za kiuchumi zitatolewa katika mfumo wa mrahaba, kodi pamoja na kupata asilimia 16 ya faida kutokana na kampuni hizo kufanya kazi nchini.

Alisema Barrick kulipa dola milioni 300 za kimarekani kwa Serikali ya Tanzania kama malipo ya Patano kuhusu fidia ya kodi kutokana na makubaliano yaliyofikiwa.

## HALMASHAURI YA MJI KAHAMA

KAHAMA TOWN COUNCIL

## TANGAZO LA ZABUNI

### Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01, LGA/155/2020/2021/G/01, LGA/155/2020/2021/W/01

1. Halmashauri ya Mji Kahama inakaribisha maombi ya Zabuni za huduma mbalimbali zisizokuwa za kitaalam(Non Consultancy Services), bidhaa(Goods) na kazi mbalimbaliza Ujenzi(Works) kutoka kwa watu binafsi,vikundi au kampuni zenye kutoa huduma hizo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 .

2. Hivyo basi Halmashauri ya Mji Kahama inakukaribisha kuleta maombi yako kwa ajili ya huduma zisizo za kitaalam, bidhaa na kaziza Ujenzi kama zilivyoelezwa kwenye orodha hapa chini.

| | |
|---|---|
| **A. ZABUNI ZA HUDUMA ZISIZO ZA KITAALAMU(Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01** | |
| 1 | Huduma za kunyonya maji taka. **Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/01** |
| 2 | Huduma ya matangazo ya sauti(public advertisement)<br><br>**Zabuni Na LGA/155/2020/2021/NC/01/02** |
| 3 | Huduma ya ulinzi kwenye majengo na ofisi za Halmashauri<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/03** |
| 4 | Huduma ya usafi kwenye majengo na ofisi za Halmashauri (VIKUNDI VYA KIJAMII)<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/04** |
| 5 | Huduma za kukarabati vifaa tiba (preventive and mantainance)<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/05** |
| 6 | Huduma ya kukodisha viti ,meza,mapambo na mahema<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/06** |
| 7 | Huduma ya ukarabati vifaa vya ofisi (ambavyo ni scanners, photocopy machine computer,printer,ups). **Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/07** |
| 8 | Huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/08** |
| 9 | Kupangisha vibanda 19 katika soko la Namanga – kodi TZS 60,000/= kwa mwezi<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/09** |
| 10 | Kupangisha meza sabini katika soko la Namanga –kodi TZS 10,000/= kwa mwezi<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/10** |
| 11 | Kuendesha choo cha Stendi Kuu ya Mabasi<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/11** |
| 12 | Huduma ya kukusanya na kusafirisha taka ngumu<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/12**<br><br>Kukusanya ada, kuzoa taka ngumu na kuzisafirisha moja kwa moja kwenda dampo la Busoka katika kata za Kagongwa, Mwendakulima, na Zongomera. |
| 13 | Kuendesha choo cha parking ya malori Majengo<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/13** |
| 14 | Kuendesha choo cha stendi ya CDT<br><br>**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/14** |
| 15 | Utangazaji stendi kuu ya mabasi ,stendi ndogo,stand ya CDT na stendi ya viwanda Dodoma. **Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/15** |
| 16 | Kupangisha vibanda sita (06) vya biashara katika Eneo la choo cha parking ya malori Majengo **Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/16.**<br>1. Waombaji wataje kodi watakazoweza kulipa kila mwezi<br>2. Waombaji wasiwe na historia ya kushindwa kulipa kodi za vibanda walivyopangishwa na Halmashauri vilivyopo maeneo mengine ya Halmashauri<br>3. Wawe tayari kufuata taratibu nyingine za zabuni kulingana na watakavyoelekezwa na kitengo cha Manunuzi |
| **B. ZABUNI ZA BIDHAA (Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/G/01** | |
| 1 | Huduma ya kuuza matofali. **Zabuni Na. LGA/155/2010/2021/G/01/01.** |
| 2 | Huduma ya kuuza mitungi ya Gesi. **Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/G/01/02** |
| 3 | Huduma ya kuuza mawe ,mchanga, kokoto na moramu. **Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/03.** |
| 4 | Huduma ya kuuza mbao na mirunda. **Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/04** |
| 5 | Huduma ya kuuza milango na madirisha ya Grill, Top na Fremu za Mbao, Madawati na madirisha ya Aluminium . **Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/NC/01/05** |
| **C. ZABUNI ZA KAZI ZA UJENZI (ZABUNI NA. LGA/155/2020/2021/W/01** | |
| 1 | Huduma ya ukandarasi(contractors pre-qualification) wa majengo,barabara,umeme,air condition na majokofu.(**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/W/01/01).** |
| 2 | Mafundi ujenzi mbalimbali(local Fundi). (**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/W/01/02.**<br>• Mwombaji awe na leseni halali ya biashara ya ufundi ujenzi |
| 3 | Mafundi wa kuchomelea (Welding). (**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/W/01/03)** |
| 4 | Mafundi umeme ambao siyo wakandarasi, mafundi selemala. (**Zabuni Na. LGA/155/2020/2021/W/01/04)** |

**3. MASHARTI KWA WAOMBAJI**

1. Mwombaji awe na leseni hai kwa biashara husika, mwombaji aonyeshe utambulisho wa mlipa kodi(TIN),usajili wa kampuni,usajili wa VAT kwa wale wanaokidhi matakwa ya kusajiliwa kwenye VAT,uhalali wa kisheria wa kusaini nyaraka (Power of attorney).
2. Mwombaji ataje kiasi cha asilimia (%) atakacholipwa na Halmashauri kutoka kwenye makusanyo.Makusanyo yote yanatakiwa kuingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri.Mwombaji atatakiwa kulipa dhamana ya mwezi mmoja kabla ya kusaaini mkataba.Afanye utafiti kabla ya chanzo kabla ya kuomba.Asiwe anadaiwa kodi ya aina yoyote na Halmashauri.
3. Kwa upande wa huduma tofauti na kukusanya mapato mwombaji ataje gharama/bei kwa huduma takayoitoa.
4. Maombi yatalipiwa ada ya uzabuni ya TZS 50,000/= ambzo hazitarejeshwa ,fedha hizi zilipwe ofisi ya mkurugenzi wa Mji,S.L.P 472 kahama,isipokuwa kwa zabuni ya kupangisha vibanda na meza zitalipiwa TZS 10,000/= kwa kila zabuni.
5. Mwombaji wa kukusanya taka ngumu anatakiwa awe na magari/trekta yenye uwezo wa kubeba tani 8 au zaidi.

   Wafanyakazi wote wawe waadilifu na wenye umri zaidi ya miaka 18 na wapewe vifaa vya kazi pamoja na nyenzo za kujikinga(viatu vigumu,kofia ngumu,ovaroli,miwani,gloves na mask) vyote vikiwa na nembo ya kampuni husika,awe na ofisi yake inayotambulika katika mji wa Kahama,awe tayari kufanya kazi katika mazingra yenye miundombinu hafifu mno;(barabara mbovu na njia zenye matope),awe na uwezo wakufanya kazi kabla kuanza kukusanya pesa angalau kwa mwezi mmoja,awe tayari kulipa ushuru wa dampo kiwango cha 15% ya makusanyo ya ushuru kila mwezi kwa mkurugenzi wa Mji wa Kahama,awasilishe bank statement ya miezi 6 ya nyuma,

   Awasilishe kadi za umiliki wa magari na vifaa vingine alivyo navyo,awe na uwezo wa kuondoa taka mbili kwa wiki toka kila kaya au jengo.

6. Vitabu vya Zabuni vinapatikana kwenye Ofisi ya Katibu wa Bodi ya Zabuni, Halmashauri ya Mji Kahama, S.L.P 472, Kahama kuanzia Saa 1.30 Asubuhi hadi Saa 9.30 Alasiri
7. Maombi yote yajazwe kwa umakini na yaambatane na nakala halisi Moja na nakala iliyorudufiwa (Copy) Moja) na yafungwe vizuri kwa lakiri na juu ya bahasha andika jina la zabuni unayoomba. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 10/06/2019 saa 5.00 asubuhi. Zabuni zitafunguliwa siku hiyo hiyo na waombaji mnakaribishwa kuhudhuria sherehe za ufunguzi.

**Maombi yote yatumwe kwa:**
**KATIBU WA BODI YA ZABUNI,**
**HALMASHAURI YA MJI,**
**S.L.P 472,**

8. Maombi yatakayochelewa au sehemu ya maombi, maombi ya kielektroniki, na maombi ambayo hayakufunguliwa kwenye sherehe ya ufunguzi wa maombi , kwa hali yoyote ile hayatapokelewa na hayatakubaliwa kwa tathmini.

**Anderson D Msumba**
**MKURUGENZI WA MJI**
**KAHAMA**

157513

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kutatua vikwazo vya uwekezaji ni muhimu

ZIMEBAKI siku 34 kabla ya kufika ukomo kwa mwaka wa fedha 2020/21. Wakati mwaka huo wa bajeti ya serikali nao ukiwa ukingoni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, amewatoa hofu wawekezaji na wafanyabiashara juu ya vikwazo vinavyowakabili.

Waziri huyo alisema juzi kuwa serikali iko katika mchakato wa kuanzisha sheria mpya ya uwekezaji, lengo likiwa ni kuhakikisha inaimarisha mazingira bora ya uwekezaji nchini.

Kwa mujibu wa waziri huyo, vikwazo vinavyowakabili wawekezaji ni pamoja na utitiri wa kodi, ukosefu wa maji ya uhakika, ubovu wa miundombinu ya barabara, gharama kubwa za uzalishaji na uzalishaji duni.

Vingine ni ugumu wa kuanzisha viwanda vidogo vya kusindika, ukosefu wa utaalamu katika kilimo na uwapo wa bidhaa zisizo na ubora sokoni.

Waziri huyo alisema pamoja na serikali kufuta kodi na tozo zaidi ya 160, itaendelea kuboresha miundombinu muhimu ikiwamo barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) na kuweka mazingira ya uhakika ya upatikanaji wa umeme.

Nipashe tunaipongeza serikali kwa kutambua umuhimu wa sekta ya uwekezaji na biashara na kuamua kuchukua hatua kutatua matatizo yanayowakabili wawekezaji kwa maendeleo ya uchumi wa nchi.

Tunatambua jitihada zinazofanywa na wizara husika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, bali pia zinaongeza nguvu katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Dira hiyo iliyozinduliwa Juni 1999, pamoja na mambo mengine, inalenga kupunguza nusu ya watu wanaoishi katika umaskini na kuwafanya wawe katika uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025.

Uamuzi wa kupitia upya sheria na sera zinazohusiana na biashara na uwekezaji nchini ni muhimu kufanyika katika kipindi hiki ambacho tayari kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wadau wa sekta hiyo, huku kukiwa na taarifa za biashara nyingi kufa na nyingine kusuasua.

Tunaamini hatua hiyo pia ni muhimu kuchukuliwa kipindi hiki ambacho nchi iko katika utekelezaji wa azma yake ya kuwa na uchumi wa kati unaochagizwa na viwanda ifikapo mwaka 2025.

Matarajio yetu ni kwamba, upitiaji wa sheria na sera zinazohusu kada ya uwekezaji na biashara pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya biashara nchini, utatatua vikwazo vya uwekezaji na kuweka mazingira mazuri yatakayowanufaisha wawekezaji na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Tunaamini mapitio haya pia yatafanywa na wataalamu wa sekta husika kwa pasi na kusahau ushirikishwaji wa wadau muhimu wa uwekezaji wa biashara ambao ndiyo walengwa namba moja wa mapitio yenyewe.


Wawekezaji na wafanyabiashara nchini mara kadhaa wamekuwa wakiziweka wazi changamoto wanazokabiliana nazo kwenye mikutano na majukwaa kadhaa ya biashara, ambapo serikali imekuwa ikiwakilishwa na maofisa wake waandamizi wakiwamo mawaziri. Kwa mfano, mwaka jana na mwanzoni mwa mwaka huu ilifanyika mikutano na majukwaa kadhaa ya uwekezaji katika mikoa mbalimbali, na wawakilishi wa serikali akiwamo waziri mkuu, waziri, makatibu wakuu na wakuu wa mikoa walihudhuria na kuahidi kuzifanyika kazi changamoto hizo.

Kadhalika, mwaka 2018, Rais John Magufuli alikutana na wawekezaji katika jukwaa la biashara kupitia Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) ambalo ni mwenyekiti wake, ambapo alipokea changamoto hizo na kuwaahidi kuzifanyia kazi.

Shime, ni muhimu nchi ichukue hatua kuzitatua kero zinazowakabili wawekezaji na wafanyabiashara nchini kipindi hiki ili kutengeneza mazingira rafiki kuelekea Tanzania yenye uchumi wa nchi unaochagizwa na ujenzi wa viwanda.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Huenda ni zama za ACT-Wazalendo kutamba upinzani

Na Ani Jozeni

WAKATI bunge linapokaribia mwisho wa shughuli zake tunapoelekea mwezi ujao, macho na masikio yanaanza kuhamia kwenye uchaguzi mkuu ambao mwaka huu unaweza kufanyika katika mazingira tofauti.

Ni kuogopa kutokana na uwepo wa ugonjwa wa corona, hivyo kuweka vizuizi vya mikusanyiko ya watu, kulingana na hali itakavyokuwa hadi kipindi cha kampeni kikianza rasmi mwezi Agosti.

Hata hivyo kinachoangaliwa sasa ni jinsi watu wanavyojipanga kugombea, na hasa wabunge walipo sasa.

Utafiti kuelekea uchaguzi mkuu unaonyesha kuwa kuchaguliwa tena katika nafasi ya ubunge si kazi ndogo, na tatizo siyo nguvu ya vyama vya upinzani ila uwezo wa mbunge husika kuwaridhisha wapigakura kuwa bado ndiye mtu sahihi kwa nafasi hiyo. Wapigakura hawana hulka ya kuchagua vyama, licha ya kampeni za miaka mingi za wanaharakati wa vyama vingi, kuwa mfumo wa viti kutokana na uwiano wa kura ndiyo utaleta demokrasia halisi.

Uchaguzi mkuu ujao hautakuwa rahisi kwa wagombea kutoka vyama vya upinzani kwa upande mmoja, na labda zaidi ya ilivyokuwa awali, hata wabunge kutoka CCM watakuwa na wasiwasi zaidi pia.

Katika kila uchaguzi mkuu kuanzia mwaka 1995, kunakuwa na chama cha upinzani ambacho kwa wakati huo kinakuwa kimejiandaa vyema zaidi kuliko wengine, hasa kwa kunasa viongozi wa kitaifa wenye mvuto kwa wapigakura.

Mwelekeo huu siyo rahisi kusema kama utafikiwa katika uchaguzi mkuu ujao au la, lakini zipo dalili kuwa ACT-Wazalendo wako tayari au wana uwezo wa kisaikolojia wa kujiandaa kupokea mtu maarufu atakayepeperusha bendera yao kwa mafanikio zaidi. Ni mtu anayemzidi 'kimo' kiongozi wa kitaifa Zitto Kabwe, avute wapigakura.

Kwa upande wa pili, unaweza kusema hakuna uwezekano wa Chadema kupata mgombea wa aina hiyo, baada ya kufarakana na kada wa CCM, Edward Lowassa, ambaye baada ya kukatwa na CCM aliendeleza 'safari ya matumaini' Chadema, hata hivyo hakuiva kiitikadi na chama hicho na akaondoka.

Kuibuka kwa Chadema kulifuatia kudorora kwa Chama cha Wananchi (CUF) baada ya uchaguzi mkuu 2005 ambako ilikuwa na matumaini makubwa kushinda urais Zanzibar na wabunge wengi. Ikatokea kuwa mgombea mwenza wa Chadema asiyefahamika Zanzibar na kwa kawaida ni mkazi wa Bagamoyo, Jumbe Rajab Jumbe, akafariki dunia siku nne kabla ya kupigwa kura, Zanzibar wakaendelea na upigaji kura lakini Bara ukaahirishwa hadi Desemba 4.

Maalim Seif alipotangazwa kushindwa Zanzibar, wafuasi wa CUF wakakosa ari Bara, na wengi hawakujitokeza kupiga kura, hivyo mgombea wa CCM akapata kura kwa asimilia 80.

Baadhi katika CCM wakatafsiri kuwa ndiyo kiwango halisi cha kupendwa chama hicho hasa kutokana na kura ya maoni ya mwaka 1991 kuhusu mfumo wa vyama vingi, ambako asilimia 80 walitaka chama kimoja, huku asilimia 20 wakipendekeza vyama vingi.

Ni kama waliotaka mfumo wa chama kimoja kimsingi wapo CCM, wakati mpangilio wa matokeo ya uchaguzi mkuu tangu mwaka 1995 yanaonyesha kuwa CCM ilikuwa inaungwa mkono kwa takriban asilimia 70 katika maeneo ya vijijini, au chini ya asilimia 50 kwa maeneo ya mijini. Hivyo wagombea upinzani wakawa wanashinda mijini tofauti, na maeneo machache zaidi vijijini.

Hali hii inaboreshwa pale upinzani unapopata kiongozi wa kitaifa anayejulikana apewe bendera ya chama kimojawapo aipeperushe, watu waone kuwa ni mbadala halisi na wenye uwezo wa utawala ukilinganisha na rais aliyeko madarakani. Hivyo hadi sasa alikuwapo Augustine Mrema mwaka 1995 wa NCCR-Mageuzi na Lowassa 2015, na 2010 Chadema ilikuwa na Katibu Mkuu Dk. Wilibrod Slaa, ambaye aliwahi kuwa kiongozi wa kitaifa wa taasisi kubwa ya dini.

Kwaupande mwingine, licha ya kukimbiwa na makada waandamizi kuanzia pale uchaguzi mkuu 2015 ulipokamilika, kwani makada wake ndiyo waliovutiwa zaidi na uzalendo wa utendaji wa awamu ya tano (hasa katika kutumbua majipu, hata kabla ya suala la makinikia), Zitto Kabwe hajawahi kuwa na migogoro ndani ya chama.

Anao washindani wake ambao walirudi CCM ila walifanya hivyo kutokana na mazingira na siyo malumbano ndani ya chama. Kwa njia hiyo anaweza akavuna kiwango kikubwa zaidi cha kuaminiwa na wapiga kura wa upinzani na hata wanaotaka kugombea ubunge ikiwa ni pamoja na walipo Chadema, hasa kama atavuta kiongozi wa kitaifa anayejulikana 'kupimana ubavu' na JPM. Ndiyo taswira inayojengeka sasa.

## HABARI KITAIFA

# Mzee wa miaka 90 ajengewa nyumba, alikuwa akilala kwenye kibanda kibovu

**Na Ndalike Sonda, PWANI**

HATIMAYE Mishee Bin Ally (90), maarufu mzee Tumbo (90), mkazi wa Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani amepata makazi mapya baada ya wasamaria wema kumjengea nyumba ya kudumu kutokana na nyumba yake ya awali kubomoka na kusababisha awe na mazingira magumu hasa nyakati za masika.


Akizungumza jana wakati akikabidhiwa nyumba hiyo, mzee Tumbo aliwashukuru wananchi waliofanikisha ujenzi huo kutoka maeneo mbalimbali nchini na kuwataka wazidi kujitolea hata kwa watu wengine wenye uhitaji.

Alisema, awali alikuwa akiishi kwenye nyumba iliyoezekwa kwa nyasi ambayo ilikuwa inavuja nyakati za masika pamoja na mwanga wa jua kupenya hadi ndani.

Kwa upande wake Mratibu wa ujenzi huo, Irene Makene, alisema nyumba hiyo imetokana na michango ya wananchi walioguswa na maisha ya mzee huyo na kujenga nyumba ya kudumu yenye chumba kimoja, choo na chumba kingine kidogo kwa ajili ya jiko.

Makene ambaye pia ni Mratibu wa Shirika la Mtandao wa Redio za Kijamii na Habari za Maendeleo Vijijini (TADIO), alisema kuwa ujenzi huo umegharimu zaidi ya shilingi milioni tatu na sasa wanakamilisha kununua kitanda na godoro ili kumkabidhi mzee huyo.

Nao baadhi ya wananchi walioshiriki kutoa mchango huo walisema, waliguswa baada ya kuona picha za makazi ya nyumba ya mzee huyo na kuwapongeza wananchi walioguswa na maisha yake na kuamua kujitolea kumsaidia kumjengea nyumba na kutaka zoezi hilo liwe endelevu kwa watu wenye uhitaji.




Nyumba ya makuti aliyokuwa akiishi Mishee Bin Ally maarufu 'Mzee Tumbo' (90), na mpya, aliyojengewa na wasamaria wema. **PICHA: MTANDAO**

# Marekebisho ya sera ya ajira mbioni kukamilika

**Na Elizabeth Zaya**

SERIKALI imesema ipo katika hatua za mwisho za kubadili sera ya ajira ili iendane na mazingira ya sasa.

Hayo yalibainishwa na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana na Ajira, Anthony Mavunde, jana wakati akizungumza katika kipindi cha kumekucha kinachorushwa na kituo cha Televisheni cha ITV.

"Tuko katika hatua za mwisho za kubadili sera ya ajira, iliandikwa zamani mwaka 2008 na haiendani na maisha ya sasa kuna sababu kuna mabadiliko makubwa ambayo yametokea katikati hapa," alisema Mavunde.

"Tunataka kutengeneza sera ya ajira ambayo itaendana na mazingira ya dunia ya leo. Kama tunavyojua ajira ni shughuli yoyote halali inayomwingizia mtu kipato," aliongeza.

Akizungumzia kuhusu programu ya kukuza ujuzi kwa vijana inayolenga kusomesha vijana hao katika vyuo mbalimbali vya ufundi pamoja na kuwatengenezea fursa za ajira, Mavunde alisema tangu serikali ilipotangaza mpango huo kumekuwa na mwitikio mkubwa.

Alisema serikali imesomesha vijana 5,598 ambao wameingia katika shughuli mbalimbali za ajira ikiwamo katika kilimo, ufundi, biashara na nyinginezo.

"Ofisi ya Waziri Mkuu katika moja ya mikakati ya kukuza fursa ya ajira kwa vijana, tulikuja na programu ya kuwajengea vijana ujuzi, tukiamini kwamba vijana wengi kupitia hii watapata fursa ya kupata ujuzi na kuutumia kutengeneza ajira zaidi baada ya kuona ombwe la wengi wao kukosa ajira wakisubiri kuajiriwa," alisema Mavunde.

"Kwa hiyo tulianza kuchukua vijana kuanzia miaka 18 ambao hawajapata fursa ya kwenda darasani mpaka wenye digrii zaidi ya moja kwa kuwapeleka kusoma katika vyuo mbalimbali vya ufundi kwa fani tofauti kwa gharama za serikali," alisema na kuendelea:

"Baada ya kumaliza tunawaundia vikundi kupitia mfuko wa maendeleo ya vijana na tunawakopesha pesa ya kupata vifaa vya kuanzia kama sehemu yao ya ajira."

Alisema programu hiyo imesaidia kwa kiwango kikubwa kuwahamasisha vijana kuingia katika shughuli nyingi za kujiajiri.

Alitaja programu nyingine ambazo wamepanga kuzitekeleza kwa vijana nchi nzima ni kuwaelimisha namna ya kuingia katika kilimo kupitia vitalu nyumba ambavyo tayari kwa baadhi ya mikoa wameshaanza.

# Mfumo wa SCGS TADB wanufaisha wakulima wadogo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) imeendelea kutoa matumaini kwa wakulima wadogo kujikwamua kiuchumi kupitia huduma yake ya Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (SCGS).

Imesema mfuko huu ni mahususi kwa wakulima, wafugaji na wavuvi katika kuwawezesha kuchangamkia fursa za uwekezaji katika mnyororo wa thamani kwa kumuwezesha mkulima kuwekeza katika sekta ya kilimo kwa kumpatia mkopo wenye masharti nafuu.

Justine, amesema mikopo hii inatolewa kwa mkulima mmoja mmoja, vikundi vilivyosajiliwa kisheria kwa lengo la kufanya shughuli za kilimo, ufugaji au uvuvi, bila kuviacha nyuma Vyama vya Ushirika/AMCOS pamoja na wanaofanya shughuli za uchakataji wa mazao yote ya chakula.

Katika jitihada za kuhakikisha inatoa huduma bora ya mikopo, Benki hiyo imeingia ushirika na benki nane kwa lengo la kufikisha huduma yake ya mikopo kwa wakulima wengi, kwa urahisi na kwa haraka zaidi. Benki hizo ni NMB, CRDB, TPB, Mucoba, Stanbic, Uchumi, FINCA na Tacoba.

"Mikopo hii ya SCGS imetoa tumaini jipya kwa wakulima wadogo kujikwamua kiuchumi. TADB imeweza kutoa mikopo mingi na kugusa maisha ya Watanzania wengi kupitia vyama mbalimbali vya AMCOS, vikundi mbali mbali na mkulima mmoja mmoja, kama takwimu zetu zinavyoonyesha."

Alisema kwa takwimu za kipindi cha mwaka mmoja na nusu toka kuanzishwa kwa SCGS Novemba 2018 mpaka Mei 2020, jumla ya Sh. billion 48.74 zimekwishatolewa. TADB kupitia benki washirika, na kuwanufaisha moja kwa moja takribani wakulima 6,589 ambapo katika hao wanawake ni 1,155 na wanaume ni 5,374 pamoja na AMCOS 39 zikiwamo AMCOS za Mtwara Cooperative Union (MAMCU) ambayo imenufaika na mkopo wa Sh. bilioni 1.086 kwa matumizi ya kujenga maghala mawili yenye ukubwa wa kuhifadhi korosho kiasi cha tani 22,000 kwa kila ghala.

Kahama Cooperative Union (KACU) imenufaika na Sh. bilioni 2 ukiwa ni mkopo kwa ajili ya shughuli za usambazaji wa dawa ya wadudu kwa wakulima wa zao la pamba nchini kote.

Rhotia AMCOS, kilichopo wilayani Karatu, kimepata mkopo wa Sh. bilioni 37.536 kwa ajili ya matumizi ya shughuli za uzalishaji wa zao la mahindi.

# Takukuru yanasa 2 TRA madai kupokea mil. 10/-

Na Jaliwason Jasson, BABATI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani Manyara, inatarajia kuwaburuza mahakamani maofisa wawili wa Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa ya Sh. mil. 10.

Uamuzi wa kuwafikisha mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili, ulitangazwa jana na Mkuu wa Takukuru mkoani hapa, Holle Makungu.

Makungu aliwataja watuhumiwa kuwa ni Subilaga Mwangama na Ojungu Mollel.

Alisema makosa yao ni kudai na kupokea rushwa ya Sh. milioni 10 kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, namba 11 ya mwaka 2007.

Alisema watuhumiwa hao ni maofisa wa TRA Mkoa wa Manyara na watafikishwa na mawakili wa Takukuru, Isdory Kyando akisaidiwa na Martin Makani.

"Uchunguzi wetu umebaini kwamba mlalamikaji jina limehifadhiwa kwa sababu za usalama ni mlipa kodi mzuri TRA Mbulu na mwaka 2018 alilipa Sh. milioni. 9.145," alisema Makungu.

Alidai Machi 2020, alipigiwa simu na washitakiwa na kutakiwa kufika ofisi za TRA, Mkoa wa Manyara zilizopo Babati na kukutana na maofisa hao wawili, ambao walimfahamisha kuwa wamefanya ukaguzi wa biashara yake na kugundua kuwa alikadiriwa vibaya. Kutokana na hali hiyo, walimtaka kulipa ongezeko la Sh. milioni 5.8.

Mfanyabiashara huyo alikubali ongezeko hilo na alianza kulipa kwa awamu.

Imedaiwa kuwa uchaguzi wa Takukuru ulibaini akiwa amelipa awamu ya kwanza alipigiwa simu na washtakiwa na kutakiwa kwenda Babati kwa ajili ya mahojiano kuhusu ulipaji kodi wa mwaka huo wa 2018 ambao tayari walishamkadiria ongezeko.

"Mlalamikaji alikutana na maofisa hao katika ofisi za TRA Babati na kujulishwa kuwa kuna ongezeko tena kwenye kodi ya biashara yake ya Sh. milioni 45," alieleza.

Alifafanua kua ongezeko hili lilimuweka kwenye wakati mgumu, lakini washtakiwa walimpoza kwa maelezo kuwa wanaweza kumpunguzia toka Sh. milioni 45 hadi Sh. milioni tisa endapo angekubali kutoa rushwa.

Uchunguzi uliendelea kubainisha kuwa mjadala uliendelea kati yao na mfanyabiashara na wakamtaka kuwapelekea Sh.milioni 10.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, akionyesha kwa waandishi wa habari jana, mali mbalimbali zinazosadikika kuwa za wizi zilizokamatwa na jeshi hilo katika msako wake uliofanyika hivi karibuni. PICHA: FRANCIS GODWIN

# Tamko kutolewa shule binafsi kuongeza gharama kisa corona

Na Romana Mallya

BAADA ya serikali kutangaza wanafunzi wa kidato cha sita kuanza masomo Juni Mosi, mwaka huu, baadhi ya shule za binafsi zinadaiwa kuwataka wazazi walipe malipo ya ziada kwa ajili ya kinga dhidi ya corona na kuwalipa wafanyakazi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Shule ya Sekondari ya St. Mary's Mazinde Juu, Sista Evetha Kilamba, iliyosambaa mtandaoni, imewataka wazazi waweke kwenye akaunti ya shule Sh. 750,000 kama malipo kwa muda ulioongezeka.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Sylvia Lupembe, imekiri kupokea malalamiko hayo ya wazazi na kuahidi kutoa ufafanuzi wakati wowote.

"Ni kweli wizara imeyaona hayo malalamiko tutatoa ufafanuzi wakati wowote hatuwezi kukaa kimya. Lakini kama serikali ilivyosema awali muongozo wa afya utatoka wakati wowote, bado unaandaliwa na wizara husika ambayo ni Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto," alisema.

Hata hivyo, akizungumza na Nipashe, Mkuu wa Shule hiyo, Sista Kilamba, alikiri taarifa hiyo ni yao, lakini alisema ilikuwa sehemu ya majadiliano kati ya shule na wazazi.

"Ni kweli taarifa ni yetu, lakini ilikuwa kwenye majadiliano kwenye makundi ya WhatsApp kati ya shule na wazazi, bado hatukuwa tumefikia muafaka, tumeshangaa kuona mitandaoni," alisema.

Taarifa hiyo ilisema: "Salamu wazazi/walezi wa kidato cha sita 2020. Naomba kuwajulisha kuwa malipo ya muda ulioongezeka ni Sh. 750,000, malipo haya yalipwe kwenye akaunti ya shule (ambayo wameitaja).

"Malipo haya ni kwa ajili ya kulipa walimu na wafanyakazi wengine, juisi ya moto inayotengenezwa shuleni hapo, kuboresha chakula."

Pia taarifa hiyo ambayo haikuwa na saini bali jina la mkuu wa shule hiyo, iliwajulisha wazazi kuwa wanatarajia kufungua Mei 30 na wanafunzi kuanza masomo siku inayofuata.

Aidha, iliwataka mwanafunzi aende na barakoa 15, vitakasa mikono vitano, chupa ya chai ya vikombe viwili, moja, mahitaji yake ya usafi wake binafsi na mwanafunzi akate nywele nyumbani kabla ya kufika shuleni.

Pia ilitaka kila mwanafunzi aandaliwe chakula chake cha kula njiani kwa sababu hawataingia hotelini.

Naye, Mkuu wa Shule ya Sekondari Bwiru Wasichana, Mectilda Shija, kupitia tangazo alilolitoa kwa wanafunzi wa kidato cha sita, ameorodhesha vitu ambavyo wanatakiwa kwenda navyo.

Katika tangazo hilo, Shija ametaka wanafunzi waende na chupa ya chai, tangawizi iliyosagwa kilo moja, limao ya unga, vitakasa mikono angalau nusu lita, barakoa za kutosha na mahitaji mengine muhimu ya shule.

Mei 21, Rais John Magufuli alitangaza kufungua kidato cha sita ili wajiandae na mitihani ya kumaliza elimu ya sekondari ya juu baada ya kufungwa tangu Machi 17 kutokana na tishio la maambukizo ya virusi vya corona.

## 'Afrika yahitaji mkakati kuvushwa kiuchumi'

Na Romana Mallya

MWENYEKITI wa Benki ya UBA, Tony Elumelu, amesema Bara la Afrika linahitaji mkakati maalum utakaovusha vyema uchumi wake baada ya ugonjwa wa corona.

Elumelu aliyasema hayo juzi wakati wa Jukwaa la Siku ya Afrika kwa mwaka 2020 lilioendeshwa mubashara kutoka mjini Lagos, nchini Nigeria na kutazamwa duniani kupitia mtandao wa Zoom.

Alisema corona imeleta umuhimu wa kuunganisha uchumi wa nchi 55 za bara la Afrika.

"Lengo la mkakati maalum iwe ni kukuza uchumi, kutengeneza ajira na kuleta maendeleo endelevu kwa watu wa Bara la Afrika," alisema.

Alisema wanahitaji kufanya mengi, kutibu wagonjwa na kufanya kazi kwa pamoja ili waweze kufanikiwa.

Jukwaa hilo liliendeshwa kwa kaulimbiu: 'Jinsi ya Kukuza Uchumi, Kutengeneza Ajira na Kuleta Maendeleo Endelevu katika kipndi cha Covid-19'.

Katika jukwaa hilo lililowashirikisha watu maarufu akiwamo, Rais wa Liberia, George Weah, Seneta na mjumbe wa Kamati ya Mambo ya Ushirikiano wa Nje wa Senate ya Marekani, Chris Coons, Elumelu alikuwa mchokoza mada.

Wengine walioshiriki ni Rais wa Benki ya Afrexim (Afreximbank) Prof. Okey Oramah; Rais wa Jukwaa la Maofisa Watendaji Wakuu wa Afrika, Amir Ben na Katibu Mtendaji wa nchi za Afrika, Caribbean na Pacific, Balozi Georges Chicoti.

Elumelu alisema Benki ya UBA inatambua ukweli kuwa Bara la Afrika liliunganishwa kwa mara ya kwanza wakati wa harakati za uhuru na baadaye nchi zilikuza ushirikiano wao kutokana na harakati hizo kiuchumi.

Akimuunga mkono Elumelu, Prof. Oramah alizungumzia umuhimu wa nchi za Afrika kutekeleza mara moja mkataba wa makubaliano ya Eneo Huru la Biashara la Afrika.

Alisema kipaumbele cha viongozi wa bara hilo kiwe ni utekelezaji wa mkataba wa makubaliano ya Eneo Huru la Biashara la Afrika.

"Ugonjwa wa corona umetuonyesha kuwa soko huru la biashara la Afrika ndiyo njia ya kusaidia kujenga upya uchumi wa bara hili baada ya corona," alisema.

Prof. Oramah aliwataka viongozi wa Afrika kuweka pembeni wasiwasi wote kuhusu mkataba wa makubaliano ya Eneo Huru la Biashara la Afrika na badala yake waanze utekelezaji wa maslahi mapana ya bara hilo.

Alisema kwa kufanya hivyo nchi za Afrika zitajenga miundo msingi ya kujitegemea kiuchumi na kuachana na utegemezi wa kuuza bidhaa ghafi mabara mengine.

Alisema uchumi wa Bara la Afrika umeathiriwa na corona kutokana na kiasi kikubwa Afrika kutegemea mauzo ya bidhaa ghafi nje ya bara hilo.

HABARI KITAIFA

# Kasi ajali za wanyamapori barabarani yamwibua waziri

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameliagiza Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa) kuongeza idadi ya mabango ya barabarani yanayoonyesha tahadhari na faini kwa madereva watakaogonga wanyamapori katika barabara ya Babati- Arusha.

Alitoa agizo hilo katika Wilaya ya Babati mkoani Manyara katika mkutano wa wadau wa uhifadhi uliowakutanisha wataalamu mbalimbali kujadili namna ya kulinda mapito asili ya wanyamapori (shoroba) pamoja na maeneo mengine muhimu ya wanyamapori ambayo yapo hatarini kutoweka kutokana na kushamiri kwa shughuli za kibinadamu.

Kanyasu alisema kukosekana kwa tahadhari hizo kunatishia kuharibika kwa ikolojia ya Tarangire na Manyara kutokana na idadi kubwa ya wanyamapori kuuawa kwa kugongwa na magari kila siku.

Kwa mujibu wa takwimu, jumla ya wanyamapori 588 wakiwamo simba na twiga waliuawa mwaka jana kwa kugongwa na magari yanayopita kwa mwendokasi katika barabara hiyo.

Kufuatia hali hiyo, Kanyasu aliitaka Tanapa kwa kushirikiana na Jumuiya ya Wanyamapori ya Burunge kukutana na Uongozi wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) ili kutekeleza agizo hilo la uongezaji mabango katika barabara hiyo.

Akizungumzia maazimio ya Mkutano huo, Kanyasu alimwagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii kuunda kikosi kazi cha wataalamu kwa ushirikiano wa ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Babati kutambua mipaka ya shoroba katika vijiji.

Pia Kanyasu alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Babati kuhakikisha maeneo ambayo tayari yanatambulika kuwa ni shoroba yalindwe ili yasiendelee kuvamiwa.

Aidha, Kanyasu alimtaka Mkuu wa Wilaya ya Babati kuhakikisha anatoa maagizo kwa uongozi wa vijiji vinavyozunguka shoroba hawagawi maeneo ambayo ni shoroba kwa wananchi kwa ajili ya shughuli za kibinadamu ikiwamo ujenzi na kilimo.

Mbali na kuweka mabango, Kanyasu alisema kuna haja ya kuweka kamera barabarani ili kupunguza vifo vya wanyamapori wanaouawa kwa kugongwa na magari yanayopita mwendokasi katika barabara hiyo.

Akitaja athari za kuziba shoroba hizo, alisema hali hiyo ikiendelea hivyo Hifadhi ya Taifa ya Tarangire itakuwa kisiwa na kuwafanya wanyamapori wakiwamo tembo ambao husafiri kwenda kuzaliana na ukoo mwingine wataanza kuzaliana ndugu kwa ndugu, hivyo kusababisha athari kubwa kijenetiki.

Mkuu wa wilaya hiyo, Elizabeth Kitundu, alisema wananchi waliopo katika maeneo ya shoroba wamekuwa wakitambua umuhimu wa maeneo hayo na wamekuwa wakitoa ushirikiano kwao.

Kutokana na hali hiyo, ninakuahidi kupitia maofisa ustawi wa jamii tutaendelea kutoa elimu kwa wanavijiji wanaoendesha shughuli za kibinadamu katika maeneo ya shoroba wafahamu kuwa ni hatari kwao, hivyo maeneo hayo yaachwe kwa ajili ya wanyamapori wakati mchakato wa kisheria ukiendelea kutekelezwa.



Mbunge wa Musoma Vijijini, mkoani Mara, Prof. Sospeter Muhongo (mwenye barakoa), akizungumza na baadhi ya wanachama wa vikundi vya wakulima jimboni kwake, waliofaidika na msaada wa majembe ya kukokotwa na ng'ombe ambayo aliwagawia wakati wa sikukuu ya Idd El Fitri juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Biteko aombwa wataalamu wa kuchoronga miamba

**Na Lucas Raphael, TABORA**

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, ameombwa kupeleka wataalamu wa miamba watakao choronga na kubaini maeneo yenye uhakika wa madini ya dhahabu, ili wachimbaji wadogo waache kuchimba kwa hisia na kupata dhahabu kwa ajili ya kujiongezea kipato cha familia na taifa.

Kauli hiyo ilitolewa na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Nzega, Amosi Kanuda, kwa waziri huyo wakati wa ziara ya siku moja iliyofanyika katika kijiji cha Isanga.

Alisema, kutokana na wachimbaji wadogo kufanya kazi ya uchimbaji bila kuwa na utaalamu wowote na dhahabu inayopatikana kuwa kidogo na kutokuwa na tija, wakipata mtu wa kuwaongoza vyema kwenye uzalishaji bora wa dhahabu wanaweze kufanya kazi kwa tija kubwa.

"Tunachoomba sasa serikali kutuletea wataalamu kwa ajili ya kuwasimamia na kuelekeza mimba iliyopo ili wachimbaji hao waweze kuchimba na kufanya biashara yenye tija kwao na taifa kwa ujumla," alisema Kanuda.

Kanuda ambaye ni mchimbaji mdogo wa dhahabu, alisema kupatikana kwa wataalamu hao kutasaidia wachimbaji kuchimba kwa malengo na serikali itapata fedha nyingi kutokana na kile kitakachopatikana kwenye mashimo hayo.

Hata hivyo, Waziri Biteko aliwataka wachimbaji hao kuwa wavumilivu katika kipindi hiki kwa kuwa mitambo ya Shirika la Madini (Stamico), ipo sehemu mbalimbali nchini ikiendelea kufanya utafiti wa madini.

Alisema, Mkoa wa Tabora, Stamico wanaendelea na utafiti Wilaya ya Igunga na baada ya kumaliza kazi hiyo wataomba mitambo hiyo ifike eneo hilo kwa ajili ya kufanya kazi ya kuchoronga miamba na kubaini ni wapi dhahabu ilipo.

Alisema zaidi ya mashine 120 zipo na zinafanya kazi sehemu mbalimbali kwa ajili ya utafiti na ukikamilika maeneo hayo itakuja maeneo hayo kwa ajili ya uchorongaji na kupima miamba badala ya kuchimba kwa hisia.

Miezi saba imeshapita baada ya serikali kutoa leseni 11 kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu kutokana na mgodi mkubwa wa zamani Resolute uliposimamisha uchimbaji na eneo hilo kwa sasa limekuwa Chuo cha Madini, tawi la Dodoma.



## Moruwasa yapata mkurugenzi mpya

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, amefanya uteuzi wa Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA).

Taarifa ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Maji, Prof. Kitila Mkumbo, imemtaja aliyeteuliwa kuwa ni Mhandisi Tamimu Twaha Katakweba (pichani).

Aidha, Prof. Mkumbo amesema kufuatia uteuzi huo, Mhandisi Katakweba anakuwa Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi wa Moruwasa.

Uteuzi huu umefanyika chini ya Sheria Namba 5 ya Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2019.

## Upatikanaji tiba saratani ngozi waimarishwa

**Na Christina Haule, MOROGORO**

CHAMA cha watu wenye ualbino (TAS) Mkoa wa Morogoro kwa kushirikiana na serikali na wadau wengine, wamefanikiwa kuimarisha upatikanaji wa tiba ya awali ya saratani ya ngozi kwenye mikoa tisa ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mwenyekiti wa TAS Mkoa wa Morogoro, Hassan Mikazi, alisema hayo jana kwenye taarifa yake aliyoitoa kwa waandishi wa habari kwamba lengo ni kufanikisha kuwapo kwa vifaa hivyo kwenye mikoa yote Tanzania ili kuwawezesha watu wote wenye ualbino na wasio na wengine kupata huduma hiyo wakiwa kwenye maeneo yao kwa wakati wakianza na mikoa hiyo tisa.

Aliitaja mikoa hiyo ni Morogoro, Lindi, Mara, Singida, Iringa, Tanga, Dodoma, Da es Salaam pamoja na Zanzibar.

Aidha, Mikazi alisema, vifaa tiba hivyo vya saratani ya ngozi awali vilizinduliwa rasmi Juni 13, 2019 katika uwanja wa Jamhuri mkoani Morogoro na kupelekwa kwenye hospitali za mikoa hiyo saba iliyotajwa nchini.

Alisema chama hicho kimefanikiwa kufanya ushawishi kwa serikali kuanza kununua mafuta kinga ya ngozi kupitia Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na baadhi ya halmashauri za wilaya nchini.

# Magereza kufungwa 'CCTV camera' kudhibiti uovu

SERIKALI imetaja mkakati wake wa kudhibiti vitendo viovu magerezani ikiwa ni pamoja na kuongeza vifaa vya upekuzi na kufunga kamera.

Majibu hayo yalitolewa bungeni jana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Rukia Kassim Ahmed.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuzuia vitendo viovu na vibaya magerezani.

Wizara hiyo ikijibu swali hilo, ilisema Jeshi la Magereza ni chombo pekee cha serikali chenye dhamana kisheria kuwapokea na kuwahifadhi wahalifu wa aina zote wanaoletwa magerezani kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za nchi.

"Pamoja na ukweli kwamba nyakati kadhaa kumekuwapo na vitendo viovu magerezani, mathalani askari kuwa na mahusiano mabaya na mfungwa, uingizaji wa vitu visivyoruhusiwa magerezani," ilisema.

Vingine ni matumizi mabaya ya nguvu dhidi ya wafungwa, wafungwa kujaribu kutoroka, kupigana, kutoleana lugha za matusi, kuharibu mali ya gereza na vitendo hivyo vimekuwa vikidhibitiwa kwa mujibu wa sheria.

Ilitaja taratibu zilizopo za magereza kuwa ni Sheria ya Magereza ya Mwaka 1967, Kanuni za Utumishi wa Jeshi la Magereza za Mwaka 1997, Kanuni za makosa Magerezani na Kanuni za kudumu za Jeshi la Magereza, toleo la 4 la Mwaka 2003.

Pia, ilisema sheria na kanuni tajwa zimeainisha aina ya makosa, hatua na adhabu zinazopaswa kuchukuliwa dhidi ya ofisa au askari wa Magereza na mfungwa au mahabusi pale inapothibitika amefanya vitendo hivyo gerezani.

"Hivyo, mpango ambao serikali kupitia Jeshi la Magereza imekuwa nao ni kuongeza vifaa vya upekuzi magerezani na kufunga CCTV-Kamera ili kubaini matendo maovu.

"Pia kuendelea kufuata sheria na kanuni tajwa ambazo zilipitishwa na Bunge lako Tukufu na kuwachukulia hatua za Kisheria wale wote watakaohusika na kufanya vitendo viovu magerezani," ilisema.




Habari na Augusta Njoji

# Wizara yakiri bei ya mifugo kuyumba

**Na Augusta Njoji, DODOMA**



WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imekiri kuwa bei za mifugo kuyumba kutokana na kudhoofu kwa mifugo wakati wa kipindi cha kiangazi kirefu kinachojitokeza sehemu nyingi hapa nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Longido (CCM), Dk. Stephen Kiruswa.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema bei ya mifugo inayumba kila wakati kwa sababu ya viangazi virefu vinavyosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Serikali haioni kuna haja ya kupanga bei elekezi kwa kilo za mifugo akiwa hai au nyama kama ilivyo kwa mazao ya kilimo mfano pamba, kahawa na korosho," alihoji.

Wizara hiyo, ilisema kiangazi hicho kinaambatana na uhaba mkubwa wa malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

"Kukosekana kwa malisho na maji kunadhoofisha afya za mifugo na kupunguza ubora wake hivyo kushusha thamani ya mifugo hiyo," ilisema.

Ilieleza kuwa mfumo wa biashara ya mifugo unaotumika nchini ni wa soko huria, bei ya mifugo hupangwa kutokana na nguvu ya soko inayotokana na kiasi cha bidhaa au ubora wa sokoni na mahitaji ya walaji.

Ilibainisha kuwa katika biashara ya mfumo huo, kuingiliwa kwa namna yoyote ya uendeshaji wa biashara hiyo kwa kuweka bei elekezi kunapingana na dhana ya soko huria na kunavuruga utaratibu na kusababisha mtikisiko na hivyo kupoteza mwelekeo wa hali ya biashara.

"Kufanya hivyo, kunaweza kuchochea kuwapo kwa biashara zilizo kinyume na sheria, kanuni na taratibu za masoko jambo ambalo sio rafiki kwa uchumi wa nchi na afya za walaji," ilisema.

Ilieleza kuwa kwa mazao ya mashambani tofauti na mifugo, kiangazi huathiri zaidi kiwango (wingi) wa mazao hayo na kwa kiasi kidogo ubora wake.

Vile vile, ilisema mazao ya pamba, kahawa na korosho ni ya biashara ambayo hali ya soko lake ni rahisi kukisia kwa kuwa inaamuliwa na bei ya soko la kimataifa tofauti ya mifugo na mazao yake.

"Katika kukabiliana na athari za ukame kwa mifugo, wizara ikishirikiana na wadau mbalimbali inaendelea kutekeleza mkakati wa upatikanaji wa malisho na maji pamoja na kukamilisha maandalizi ya miongozo ya usimamizi wa rasilimali hizo," ilisema.

Hata hivyo, ilisema katika mwaka 2019/20, wizara imewezesha elimu ya uzalishaji wa malisho kwa vitendo katika halmashauri 11, jumla ya mashamba darasa 25 ya malisho yameanzishwa na wafugaji 685 wamepata elimu ya kilimo cha malisho kwa vitendo.

"Wizara inatekeleza hatua za awali kwa ajili ya ujenzi wa malambo matatu katika vijiji vya Chamakweza (Chalinze), Kimokoa (Longido) na Narakauo (Simanjiro) na ukarabati wa malambo matatu katika vijiji vya Kimana (Kiteto), Narakauo (Simanjiro) na Kimokoa (Longido)," ilisema.

Wizara ilibainisha kuwa imechimba visima virefu viwili katika Vijiji vya Mpapa (Manyoni) na Nsolanga-Ismani (Iringa).

"Wizara imeendelea kuweka mkazo wa kuuza na kununua mifugo minadani kwa kutumia mizani ili kumwezesha mfugaji kupata bei nzuri yenye tija, uwazi na ushindani sokoni," ilisema.

Pia, ilisema imesimika mizani katika minada 11 ya upili na mipakani na kuagiza halmashauri kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mkoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kuhakikisha minada yote ya awali inasimikwa mizani ili kuwezesha wafugaji na wafanyabiashara kupanga bei kulingana na uzito wa mnyama.

# Wafanyabiashara watungiwa kanuni usajili

BUNGE limeelezwa kuwa serikali imetunga kanuni za usimamizi wa kodi kwa ajili ya usajili wa wafanyabiashara wadogo na watoa huduma za mwaka 2020.



Hayo yalielezwa jana bungeni na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Asha Juma.

Mbunge huyo alisema zoezi la kuwapatia vitambulisho wajasiriamali wamachinga limefanyika vizuri na kuendelea kufanya biashara zao mahali popote.

"Serikali imejipanga vipi ili kuhakikisha kuwa na usimamizi na udhibiti katika ufanyaji wa biashara holela," alihoji.


Katika majibu ya ofisi hiyo, ilisema serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na ofisi hiyo imetunga kanuni hizo.

Ilisema kwa mujibu wa kanuni hizo, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimeelekezwa kusimamia na kutenga maeneo kwa ajili ya wafanyabiashara na watoa huduma wadogo ili kuhakikisha biashara holela zinadhibitiwa.

"Udhibiti na usimamizi utafanyika wakati wa kusajili na kuwapatia vitambulisho wajasiriamali wadogo kwa lengo la kuwawezesha kiuchumi na kuhakikisha wanaendesha shughuli zao pasipo kubughudhiwa," ilisema.

Ilieleza kuwa, serikali pia imeandaa mwongozo wa usimamizi wa wafanyabiashara wadogo na watoa huduma wadogo ambao umeainisha majukumu ya kila mdau katika usimamizi wao.

Licha kukandamizwa, kunyanyaswa kijinsia wanawake wameruka viunzi



Ukurasa 13



Ukurasa 12

## Wachambuzi wawatabiria heri waliotangaza kuvihama vyama

siasa
JUMATANO MEI 27, 2020
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe

# Kukosa itikadi, sera, njaa chanzo hamahama wanasiasa upinzani

**Na Gaudensia Mngumi**

SIASA za majitaka au za kuchafuana, kushambulia viongozi na kwa ujumla kuongea kila baya kuhusu chama unachokikimbia baada ya kukitumikia kwa miaka kadhaa, zinapamba moto wakati huu taifa linapoelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2020.

Sarakasi za kuvihama vyama zinaonekana zaidi upande wa vyama vya upinzani ambako wabunge wengi wamevikimbia pamoja na madiwani wakijiunga na chama tawala au kurudia kwenye upinzani ambako awali ndiko walipotokea.

Ni kitu gani kinawasukuma kufanya hivyo? Nipashe inazungumza na Dk. Sabato Nyamsenda wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kujua sababu za wabunge wengi wa upinzani kuendeleza siasa za maji taka na kuvikimbia vyama vyao kipindi hiki, wakati imesalia miezi mitano kabla ya kufanyika uchaguzi mkuu.

Nyamsenda mtaalamu wa sayansi za siasa, anasema si jambo baya kuhama chama, wanaofanya hivyo hawajakosea wako sahihi. Aidha, ni haki ya mwanasiasa kufanya hivyo ni kikatiba na kidemokrasia.

Anasema anaweza kuhama chama wakati wowote anapotaka kufanya hivyo na hazuiliwi na sheria na kwa Tanzania si jambo jipya.

Anataja mfano wa Waziri wa zamani wa Mambo ya Ndani, Augustine Mrema, alipoondoka CCM alitangaza kujiunga na TLP, lakini baadaye kwa sababu alizozijua mwenyewe alihamia NCCR-Mageuzi, pengine baada ya kutimiza masharti aliyokipa chama hicho.

Lakini baada ya mgogoro wa NCCR-Mageuzi alirudi TLP na hadi sasa anaendelea kukiongoza.

Wanasiasa na wanachama wengi wamekuwa wakihama kutoka chama kimoja kwenda kingine mfano Tambwe Hiza alikuwa CUF akahamia CCM na baadaye alijiunga na Chadema.



Mbunge wa Babati Mjini, Paulina Gekul ni miongoni mwa wabunge waliovihama vyama vyao. **PICHA: MTANDAO**

Aidha, Steven Wassira aliwahi kuondoka CCM na kuhamia NCCR-Mageuzi mwaka 1995 na kurudi tena CCM akawa mbunge na waziri pia. Kihistoria ni mambo yaliyotokea na hata sasa yanaendelea, anasema mhadhiri huyo.

### CHANZO CHA KUHAMA

Anakumbusha kuwa wanasiasa kuhama vyama vyao na kujiunga na chama tawala ni wimbi lililoanza tangu kufanyika uchaguzi mkuu wa vyama vingi 1995 hata hivyo kuhama huko kunatokana na sababu kadhaa ikiwamo kukosekana kwa itikadi na misimamo maalumu ya kusimamia katika chama wanachojiunga nacho.

Anafafanua kuwa hakuna kinachowafunga kubaki ndani ya chama kwa sababu hakuna itikidi au 'ideology' wanayoitetea na kuwaweka pamoja. Upungufu huo unawafanya kuondoka wakati wowote wakitaka.

"Hawajifungi wala kubanwa na misimamo, wala itikadi au sera ambayo inawalazimu kuisimamia na kuitetea wakati wote. Hilo halipo ndiyo maana wanaona kuhama ni rahisi na ndiyo mlango wa kutumia kutafuta fursa nyingine za kisiasa kwenye chama wanachokikimbilia," anasema mtaalamu huyo.

Anataja mfano wa Rais wa zamani wa Afrika Kusini Nelson Mandela, kama mwanachama wa ANC, alikuwa na itikadi na masuala anayoyasimamia, kutetea na kuyaendeleza hivyo, hangeweza kuhama chama kwa namna yoyote.

Hata hivyo, kwenye mataifa ambayo demokrasia zimekomaa chama kina mambo ya msingi ya kuyasimamia hivyo si rahisi mwanachama wa chama kingine kubadili misimamo na kuingia kwenye chama cha wenzake ambacho binafsi hasimamii itikadi wala maono yao.

### KUSAKA MADARAKA

Kujiongeza ili kupata madaraka kunaweza kuwa sababu ya kukihama chama ili kupata fursa zaidi. Vyama vinatumiwa kama milango au ngazi ya kupanda juu zaidi, anaeleza Nyamsenda.

Anakumbusha kuwa kwa sababu hakuna itikadi au sera mahsusi wanayoitetea wanasiasa hao kivutio chao ni kusaka madaraka kwa hiyo chama ni ngazi inayotumiwa kufikia hatima hiyo. Kwa hiyo kinachoendelea ni kuangalia ngazi ikiwa fupi au mbovu ni kuachana nayo.

Anafafanua kuwa hama hama ya kurudi CCM ni kutazamia kupata madaraka au ubunge kuliko kubaki au kwenda kwenye vyama vingine vinavyoonekana kuwa havina fursa.

Inamaanisha kuwa kwa sehemu kubwa wanasiasa waliingia kwenye siasa kutafuta fursa au madaraka na si kwamba kuna itikadi au sera walizokuwa wakizisimamia, anasema.

### MAZINGIRA MAGUMU

Nyamsenda anataja sababu nyingine inayowakimbiza wanasiasa wa upinzani wanaokimbilia chama tawala kuwa ni kujikuta katika mazingira ya kisiasa yanayowabana sana.

Hilo limetokana na kubanwa kwa shughuli za kisiasa kwa upande wa upinzani hatua inayowafanya wasione fursa upande wao na kuzifuata upande wa chama dola.

Kwa hiyo wanatumia kuhama kama mlango wa kutafuta fursa za kisiasa kwa vile milango yao imefungwa na ni vigumu kuendesha shughuli za kisiasa zama hizi.

### SI JAMBO BORA

Msomi na mwanasiasa mmoja maarufu kutoka chama tawala (jina linahifadhiwa) anaelezea hatua ya kuvihama vyama kuwa ni kitu kilichokuwapo tangu kuanza mageuzi ya vyama vingi Afrika mapema miaka ya 1990.

Anasema licha ya kuwapo kwa mfumo huo wa vyama vingi kwa miaka 30 sasa serikali nyingi za Afrika hazijaona umuhimu wa kukomesha au kudhibiti tabia ya kuvihama vyama au kuanzisha vingine, ikibidi kwa kutunga sheria au kuweka kanuni za kuwabana wanaohama.

# Wachambuzi wawatabiria heri waliotangaza kuvihama vyama



Seif Shariff Hamad ni miongoni mwa wana CUF waliokikimbia chama hicho kutokana na migogoro na kujiunga na ACT- Wazalendo. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Sabato Kasika**

KILA mwaka wa uchaguzi, huwa kuna pilika nyingi zikiwamo za baadhi ya wanasiasa kuhama vyama vyao vya awali na kujiunga na vingine. Huchukua hatua hiyo kwa madai kuwa wana haki ya kufanya hivyo na hawavunji sheria.

Wawe wameahidiwa chochote kule wanakohamia au wamekorofishana na viongozi wao huko wanakotoka, msingi wao mkuu na wa kwanza ni kutafuta madaraka.

Kwa hiyo huo ndiyo wakati wa kuhangaika huku na kule, kutumia kila mbinu za kila namna zikiwamo chafu kuhakikisha wanapata wanachotaka bila kujali wameumiza wengine katika safari yao ya kusaka madaraka.

Baadhi ya wanasiasa wameanza safari hiyo kwa kutangaza kuvihama vyama vyao vya awali wakisubiri bunge kuvunjwa ili waende kule ambako wameomba kuhamia.

Wapo wabunge wa vyama vya upinzani waliotangaza kuhama vyama vyao na kuhamia vingine ndani ya upinzani, huku wakiwamo wa upinzani waliotangaza kuhamia CCM.

Kwa mfano wabunge Joseph Selasini (Rombo) na Anthony Komu (Moshi Vijijini) wote wa Chadema wameshatangaza kujiunga na NCCR- Mageuzi.

Katika safari hiyo ya kwenda NCCR- Mageuzi, wamo pia wabunge wa viti maalum wa Chadema, Joyce Sokombi na Susan Masele, huku mbunge mwingine Peter Lijualikali (Kilombero), ameomba kujiunga na CCM.

**UTABIRI WA HATIMA**

Kutokana na hatua hiyo ya wabunge kutangaza kuhama, baadhi ya wanasiasa na wachambuzi wa mambo ya siasa wamekuwa na maoni yao, huku wengine wakidai kwamba mambo ya siasa Tanzania hayajawa kwenye mstari ulionyooka.

> “Ndani ya upinzani hali si shwari kutokana na mgawanyiko ambao haukupaswa kuwapo wakati huu ambao nchi inaelekea kwenye uchaguzi mkuu kwani hauna afya kwenye siasa.



Mbunge Joseph Selasini ametangaza kuhama Chadema na kurejea ‘nyumbani’ NCCR-Mageuzi. **PICHA: MTANDAO.**

Thomas Ngawaiya ni mwanasiasa mkongwe nchini, ambaye anaona, kuna udhaifu kwa wanasiasa na kukosa msimamo ingawa kila mmoja ana haki ya kuhama chama kimoja kwenda kingine.

“Demokrasia ni kama mchezo wa kuigiza, kwani ukiuliza kwa nini wanahama, utasikia wanagombana kwa sababu ya maslahi badala ya kutafutia wananchi demokrasia ingawa kikatiba kuhama ni sawa,” anasema Ngawaiya.

Pamoja na hayo, mwanasiasa huyo anasema, wakati mwingine kuyumba kwa vyama vya upinzani kunasababisha hayo yote, kwa vile mwanachama anakaa muda mrefu bila kuona mabadiliko yoyote anamua kuondoka.

Ngawaiya ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji Mtendaji wa Taasisi ya Utawala Bora na Maendeleo Tanzania (Cegodeta), anatoa ushauri kwa upinzani kutafuta mbinu nyingine za kutoka upya, vinginevyo utaendelea kuyumba.

**NI KUFA UA KUPONE**

Wakati Ngawaiya akisema hayo, mchambuzi wa masuala ya siasa nchini, Abdulkarim Atiki, anasema siasa ina mchezo wake ambao wakati mwingine mwanasiasa akiucheza vibaya anaweza kuumia.

“Nimewasikia wanasiasa waliotangaza kuhama vyama vyao baada ya bunge kuvunjwa, sasa yawezekana wakawa wamechanga vizuri karata wakafanikiwa katika uchaguzi ujao au wakafa kisiasa,” anasema Atiki.

Anafafanua kuwa katika siasa, kuna wanaoshinda uchaguzi kutokana na ushawishi wao na wengine wanashinda kutokana na nguvu ya vyama walivyopitia, hivyo hayo yote yanaweza kutoa majibu.

“Mwanasiasa aliyepata ushindi kwa nguvu ya chama inakuwa vigumu kupata ushindi huo kupitia chama kingine, lakini kama ni kwa ushawishi wake, hilo halina shida kabisa,” anasema.

Anasema, mara nyingi mbunge au diwani kuhama huwa anawachanganya wapigakura na kushindwa kuamua kama wamfuate au wabaki kwenye chaka walichopitia kupata ushindi.

Anasema, wengi wa wanasiasa hushindwa kwa nguvu za vyama, hivyo anaona kwamba wapo waliohama watakaopitishwa na vyama vipya na kushinda au kutoswa na kupotea kisiasa.

**MIGOGORO KUFURUKUTA**

“Ukifuatilia kwa umakini utabaini wale waliotangaza kuhama, wana migogoro kwenye vyama vyao vya awali, wanaondoka wakiwa hawana baraka za vyama vyao, hilo ni tatizo katika siasa wanaweza wakapotea kisiasa,” anasema Atiki.

Anaeleza kuwa matendo ya wanasiasa yanazungumza zaidi kuliko sauti zao zinavyosikika kila mara mbele ya wananchi, hivyo wanaweza kufanikiwa au kupotea kisiasa kutokana na matendo yao.

Atiki anasema, baadhi ya vyama vya upinzani huwa vinadai kuhujumiwa na CCM, lakini anafafanua kuwa migogoro katika vyama hivyo ndiyo mwanzo wa kukimbiwa na wanachama.

“Katika siasa, mchezo mchafu upo, lakini siyo kama hivyo ambavyo vyama vya upinzani vinalalamika, bila kujua kuwa vinajua vyenyewe, kwa sababu ya migogoro isiyo ya lazima,” anasema Atiki.

Mchambuzi huyo anaeleza kuwa wakati huu wa kuelekea kwenye uchaguzi mkuu, vyama vingejikita zaidi katika kuimarisha umoja, lakini badala yake vinakuwa na malumbano hadi kufukuzana.

“Ndani ya upinzani hali si shwari kutokana na mgawanyiko ambao haukupaswa kuwapo wakati huu ambao nchi inaelekea kwenye uchaguzi mkuu kwani hauna afya kwenye siasa,” anasema.

Anaeleza kuwa kwa mtindo huo unasababisha vingine katika uchaguzi vikiwa vimesambaratika vyenyewe badala ya kuwa na umoja ambao ungevivusha hadi kufikia ushindi kama ilivyotokea mwaka 2015.

“Wabunge waliochaguliwa mwaka 2015 vipindi vyao vinamalizika mwaka huu wa 2020, wapo ambao wanataka kuendelea kuongoza na wengine wametangaza kustaafu, hao wanaoendelea inabidi wajipange vizuri,” anasema.

Anasema, mara nyingi mbunge au diwani kuhama kunawachanganya wapigakura na kushindwa kuelewa kama wamfuate au watafute mwingine.

# Licha kukandamizwa, kunyanyaswa kijinsia wanawake wameruka viunzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA



Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Kahama, Thelesphora Saria, akizungumza na Nipashe. **PICHA: SHABAN NJIA**

MWANAMKE katika jamii nyingi nchini kwa miongo kadhaa hakuthaminika kwenye masuala mengi ikiwamo elimu ambayo ni msingi mkubwa wa kila kitu.

Elimu ndiyo inayokuwezesha kuingia kwenye siasa au kupata mwanga wa kushiriki kwenye uongozi uwe wa kifamilia, kitaifa au kwenye ngazi zozote.

Kwa wanawake wengi mila potofu zimewanyima fursa ya kujitokeza kugombania nafasi za uongozi kwenye jamii na wakati mwingine zimewaangusha na kubakia kwenye nafasi za uteuzi hasa eneo la siasa.

Mwanamke au binti huchukuliwa kama mtaji wa familia atakayeozwa kwa kubadilishana hasa ng'ombe, wakati mwanaume, anaendelea kuthaminiwa kwa kila kitu. Anapewa elimu, mali na heshima kwa kuwa ndiye anayeonekana kuwa mwenye enzi ndani ya jamii yake.

Lakini, Wilaya ya Kahama iliyoko mkoani Shinyanga ina ujumbe wa kuhamasisha wanawake wa kanda ya ziwa ambao kwa kiasi kikubwa jamii za ukanda huo hazithamini wala kuenzi mchango wanawake.

Ndani ya wilaya hiyo kuna kata 58 na majimbo matatu ya uchaguzi. Wilaya nyingine ni Ushetu ina kata 2 huku Jimbo la Msalala likiwa na kata 18. Zote hizo madiwani wanawake kwenye kata wakiwa wanne pekee.

Msalala wako wawili, Ushetu kuna mmoja na Halmashauri ya Mji wa Kahama yuko mmoja ambaye ni Mary Manyambo na huyo ndiye Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri.

Madiwani hao akiwamo Manyambo waliopata nafasi hizo, baada ya kuwa kwenye viti maalumu kwa muda mrefu na vuguvugu la usawa wa kijinsia la 50/50 lilipoanza chama kiliwasimamia kwa nguvu zote na kufanikiwa kupata nafasi hizo mpaka sasa wanaelekea kumaliza muda wao.

### HISIA ZA DIWANI

Marry Manyambo ni diwani wa kata ya Kinaga Halmashauri ya Mji wa Kahama, ambaye katika mahojiano na Nipashe anakiri kuwa kuwapo kwa mila potofu kwenye jamii nyingi za ukanda wa ziwa kumewanyima wanawake frusa za kugombea nafasi za uongozi ndani ya jamii.

Manyambo anasema: "Kabla ya watoto wa kike au mwanamke kupewa elimu alikuwa haruhusiwi kujieleza ndani ya familia anayotoka hata kama alikuwa na hoja zenye kuleta mabadiliko. Hali hiyo ilisababisha kuwaeleza watoto wa kiume kuwasemea."

Anaongeza kuwa ukikuta mwanamke kwenye jamii ni kiuongozi basi anakuwa mtendaji wa kijiji au kata kutoka mikoa mingine na wakati mwingine ilikuwa lazima apate changamoto hasa pale anapowasilisha hoja na kushindwa kuungwa mkono kwa kigezo ni mwanamke.

Anaendelea: "Mambo yamebadilika baada ya serikali kutoa fursa kwa mabinti na kinamama kusoma na kuelewa haki zao na

> Mwaka 2004 alijiunga na CCM na kuanza harakati za kisiasa na kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa UWT wa Kata na aliongoza umoja huo na kusisitiza haki kwa kila mmoja.



Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Kahama ambaye ni Diwani wa Kata ya Kinaga, Mary Manyambo akizungumza wakati wa kikao cha Baraza la Madiwani.

kusababisha wengi wao kutambua kuwa wanahaki za kujiunga na chama chochote hapa na kugombea nafasi za uongozi wanaanza kujitokeza."

Anasema mwaka 2004 alijiunga na CCM na kuanza harakati za kisiasa na kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa UWT wa Kata na aliongoza umoja huo na kusisitiza haki kwa kila mmoja.

Anasema mwaka 2005 aliombwa na wananchi wa kata hiyo kugombea udiwani na alikuwa na uzoefu kuanzia ndani ya chama hakuona kama kunaugumu wa kushindwa kugombania nafasi hiyo na wanaume.

"Mwaka huo, chama kilinipitisha na kuwa mgombea udiwani wa kata na nilishinda kwa kishindo kwa kuwashinda wapinzani na nilitumia kigezo cha mwanamke mjane kwenye jamii ana uwezo mkubwa kuliko mwanaume wa kulea familia ambayo ameachiwa na mke," anasema.

Manyambo anaendelea kusema, mwaka 2010 alijitosa kutetea nafasi yake ya udiwani na aliipata kutokana na yale aliyokuwa ameyafanya kwenye miaka mitano iliyopita hasa kwenye sekta ya kilimo, afya, elimu, barabara pamoja na maji.

Aidha, anasema kuwa, mwaka 2015 pia alichaguliwa kwa mara nyingine na kuchukua maamuzi magumu ya kugombea nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, ambapo pia alishinda nafasi hiyo kwa kishindo na mpaka sasa ni kiongozi.

### ELIMU KATA

Manyambo anasema kuwa, kabla ya kata kugawanywa alikuwa akiongoza kata mbili ya Kinaga na Mwanase na kwa sasa kata hiyo ipo Halmashauri ya Msalala na anakumbusha kuwa aliwahamasisha wananchi kujenga shule za sekondari mbili na za msingi tano.

Anasema kuwa, baada ya kugawanywa kwa kata ya Kinaga na Mwanase kuwa kata moja ya sekondari ilibaki Mwanase na sasa wamechangishana kila kaya Sh. 10,000 kujenga sekondari mpya ambayo inasubiri kukamilishwa na serikali baada ya kujengwa hadi lenta.

Aidha, anasema kuwa, kata anayoongoza ina vijiji vitano na kila kijiji amehakikisha kina shule ya msingi, vijiji hivyo ni Kianga na Magobeko.

### MWENYEKITI UWT

Thelesphora Saria ni Mwenyekiti wa UWT Wilaya ya Kahama anasema kuwa, kila ifikapo mwaka wa uchaguzi mkuu na uchaguzi wa ndani ya chama wamekuwa wakiwahamasisha wanawake kujitokeza na kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

Anasema kuwa, Wilaya ya Kahama ina madiwani wanawake wanne wenye kata kutoka Halmashauri za Msalala, Kahama Mjini na Ushetu na wamekuwa wakiwahamasisha kugombea nafasi za ubunge viti maalumu au ubunge wa wajimbo.

Aidha, Saria anasema kuwa, wakiwa kwenye mikutano yao ya kinamama ya kichama, amekuwa akiwahamasisha wanawake kujitoa na kugombea nafasi za uongozi kwa kutumia mifano ya viongozi wa kitaifa wanawake kama vile Waziri wa Afya Ummy Mwalimu na Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Pia, anasema kuwa, viongozi wanawake kwenye jamii wamekuwa wakifanya kazi kikamilifu ikilinganishwa na kinababa au vijana hasa kwenye masuala ya elimu, afya, maji na barabara kwa kujitoa na kuhakikisha wanatatua kero za wananchi au wapigakura wao.

Mwenyekiti wa UWT anasema hataki kuona madiwani wa viti maalumu wakiendelea kugombea nafasi hizo na kukaa kwa vipindi virefu na badala yake anawahamasisha waingie kwenye kinyang'anyiro cha kugombea uongozi kwenye kata kwa kuwa wana uzoefu wa namna ya kuwahudumia wananchi na wameshiriki kwenye uongozi kwa kipindi cha kutosha.

Pia, anaeleza kuwa, amekuwa akipokea malalamiko mengi kutoka kwa madiwani wanaume wenye kata kuwa wanaingiliwa na madiwani wa viti maalumu kwenye majukumu yao, na hii ni kutokana na madiwani hao kujisahau na kusaidiwa na kinamama katika kutekeleza majukumu yao.

EVARISTE NDAYISHIMIYE

# Mjeshi wa Burundi anatinga madarakani kidemokrasia



Evariste Ndayishimiye katika kampeni za uchaguzi. **PICHA: AFP**

**Na Mashaka Mgeta**

LILIKUWA suala la kusubiri muda tu, kuiona Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (CENI) nchini Burundi, ikimtangaza mgombea urais kupitia chama tawala cha CNN/FDD, Meja Jenerali mstaafu Evariste Ndayishimiye, kumrithi Rais Pierre Nkurunziza anayeondoka.

Anaondoka Ikulu baada ya kuitawala nchi hiyo kwa miaka 15.

Ni matokeo ya uchaguzi uliotokana na kampeni zilizotawaliwa na vurugu, huku wapinzani wakilalamika mara kwa mara kufanyiwa vurugu na kukamatwa kiholela.

Kwa mujibu wa CENI iliyotangaza matokeo hayo chini ya ulinzi mkali wa maofisa wa jeshi la nchi hiyo, Ndayishimiye alipata ushindi kwa asilimia 68.72 ya kura zilizopigwa akifuatiwa na Agathon Rwasa wa National Freedom Council (CNL) anayedaiwa kuwavutia Warundi wengi wakati wa kampeni, naye akiambulia asilimia 24.19 na wagombea wengine watano wakipata chini ya asilimia tano kwa pamoja.

Matokeo rasmi yanayomwidhinisha Ndayishimiye mwenye umri wa miaka 52 kuwa Rais wa Burundi, yanatarajiwa kuchapishwa wiki ijayo Ijumaa Juni 4.

> Matokeo rasmi yanayomwidhinisha Ndayishimiye mwenye umri wa miaka 52 kuwa Rais wa Burundi, yanatarajiwa kuchapishwa wiki ijayo Ijumaa Juni 4.

### MAREHEMU WALITUMIKA

CNL inadai kuwa matokeo yaliyotangazwa na CENI 'yamechakachukuliwa' na kwamba matokeo halisi yanatoa ushindi kwa Rwasa, hivyo safari ya kwenda kuyapinga mahakamani ni jambo lisiloepukika.

Mbali na wizi wa kura, CNL inadai kuwa wafuasi wa CNDD/FDD walishiriki kupiga kura zaidi ya mara moja na kutumia majina ya watu waliofariki na wakimbizi, kufanikisha azma ya 'kuchakachua' matokeo.

Mshauri Mkuu wa Serikali ya Burundi, Willy Nyamitwe, ambaye ni miongoni mwa viongozi wa CNDD-FDD, amekaririwa akisema hatua ya kupinga matokea hayo haiakisi matakwa ya kidemokrasia na kuwa sawa na kukosa uwajibikaji kwa taifa.

Mbali na ushindi huo wa urais, CNDD-FDD imetwaa viti 72 katika bunge la seneti wakati chama cha CNL kina viti 27 na chama cha Uprona cha Makamu wa Kwanza wa Rais anayemaliza muda wake, Gaston Sindimwo, kimepata kiti kimoja.

### ANAKOTOKA NDAYISHIMIYE

Ndayishimiye ni miongoni mwa waliokuwa waasi wa CNDD-FDD waliojiunga na kundi hilo, tena aliponusurika katika mauaji ya kikabila ya wanafunzi Wahutu katika Chuo Kikuu cha Burundi mwaka 1995, baada ya mauaji ya aliyekuwa Rais wa kwanza kutoka kwa jamii ya Wahutu, Melchior Ndadaye.

Ndadaye alikuwa Rais wa kwanza kushiriki uchaguzi wa kidemokrasia huko Burundi mwaka 1993 na pia akiwa Mhutu wa kwanza kushinda kiti hicho.

Aliuawa Oktoba 21, 1993. Hivyo alikaa madarakani kwa takribani miezi mitatu tu.

Baadaye kundi la CNDD-FDD lilibadilishwa na kuwa chama cha kisiasa ambacho kilianza kushiriki katika mazungumzo ya amani mjini Arusha mwaka wa 2000 na kuafikiana kuhusu usitishwaji wa vita.

Wakati kundi la waasi la CNDD-FDD lilipojiunga na serikali mwaka wa 2003, Ndayishimiye alikuwa Meja Jenerali, na akapelekwa makao makuu ya jeshi la taifa hilo.

Baada ya Nkurunziza kushinda uchaguzi mkuu wa 2005, alimteua Ndayishimiye kuwa Waziri wa Usalama wa Ndani na Usalama wa Umma, na badaye kuhamishwa ofisi ya Rais mwaka 2007 akiwa mshauri wa kijeshi.

### NI MTU ASIYETABIRIKA

Wakati wa mgogoro ulioikumba Burundi mwaka 2015 kufuatia jaribio la mapinduzi, Ndayishimiye ni miongoni mwa viongozi wachache waandamizi jeshini ambao hawakutajwa na mashiriki ya kimataifa, kwamba walishiriki katika uhalifu dhidi ya binadamu.

Ingawa Ndayishimiye aliyezaliwa mwaka 1968 katika mkoa wa Gitega, eneo la kati mwa Burundi anaelezewa kuwa mwanasiasa mwenye msimamo wa kati, wapo wanaoamini kwamba mara nyingine hatababiriki katika hoja anazozisimamia.

Mdadisi wa kisiasa na mwandishi wa vitabu nchini Burundi David Gakunzi, anasema tabia ya kutotabirika huenda ikawashawishi wapinzani kumuunga mkono, ingawa kwa shingo upande.

"Kwa mfano, Ndayishimiye mwanzo alipinga uamuzi wa Rais Nkurunziza wa kutaka kugombea urais kwa muhula wa tatu mwaka wa 2015, ingawa baadaye alibadilisha nia na kumuunga mkono," anasema Gakunzi na kukaririwa na BBC.

Wakati hali ikiwa hivyo, mgombea aliyetoa ushindani wa karibu katika kampeni za uchaguzi huo, Rwasa wa CNL ametangaza kutoyakubali matokeo hayo akidai kuwa, pamoja na mambo mengine, uchaguzi huo uligubikwa na udanganyifu na wizi wa kura uliofanywa na watawala wa Burundi.

Kwa upande wake, CENI imeeleza kuwa 'milango ipo wazi' kwa mgombea yeyote kuwasilisha shauri lake kwenye mahakama ya katiba kwa mujibu wa sheria za nchi hiyo.

Ndayishimiye anakuwa rais wa tatu kuchaguliwa kwa njia ya kidemokrasia baada ya mtangulizi wake anayeondoka madarakani, Nkurunziza aliposhiriki Uchaguzi Mkuu wa 2005, 2010 na 2015) na Melchior Ndadaye aliyechaguliwa mwaka 1993.

Kutokana na ushindi huo, Ndayishimiye anasubiri kuthibitishwa na mahakama ya katiba na hivyo kuwa Rais rasmi wa taifa hilo dogo katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Ndiyashimiye ni mmoja wa wanasiasa wenye ushawishi mkubwa katika CNDD/FDD, na wenye ushirikiano wa karibu sana na Nkurunziza.

Kwa hiyo licha ya kuondoka Ikulu Nkurunziza bado yupo Madarakani na amepewa cheo cha "mshauri wa ngazi ya juu wa uzalendo", hali inayotafsiriwa na wachambuzi wa mambo ya kisiasa kuwa itamwezesha kuwa na ushawishi katika siasa na utawala wa nchi hiyo na akatunukiwa Dola 540,000 za Marekani na makazi ya kifahari.

Hata hivyo, anaondoka madarakani huku miongoni mwa kumbukumbu za mafanikio ya utawala wake kwa Warundi zikiwa ni kuanzisha elimu ya msingi bure, huduma bure za matibabu kwa wanawake na watoto, na kujenga barabara na hospitali.

### VURUGU

Tangu kuanza kwa kampeni za uchaguzi huo, vurugu zilizorekodiwa ziliwekwa kwenye orodha ya viashiria vya kuthibitisha kuwa huenda uchaguzi mkuu huo ungekuwa na dosari, licha ya kufanyika katikati ya corona.

Uchaguzi Mkuu wa Burundi ulifanyika wakati dunia ikiwa katika 'vita kubwa' ya kudhibiti kusambaa kwa virusi vya corona moja ya vyanzo vya maambukizo yake ni mikusanyiko kama iliyotokea wakati wa kampeni za uchaguzi huo.

Hali hiyo iliendana na tamko la serikali kuweka sharti la kuwatenga waangalizi wa kigeni kwa siku 14 tangu siku ya kuwasili kwao, hali iliyotafsiriwa kama kuwazuia wasishiriki katika uchaguzi huo.



# Taasisi zaombwa kusaidia wenye kipato cha chini

**Na Peter Mkwavila, KONDOA**

MGANGA Mfawidhi wa Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kondoa, Dk. Fransis Mwita, ameziomba taasisi mbalimbali ikiwamo mashirika ya dini na watu binafsi kuisaidia serikali katika kutatua changamoto zinazowakabili Watanzania wenye kipato cha chini.

Dk. Mwita alisema hayo alipokuwa akipokea misaada iliyotolewa na kiongozi wa madhehebu ya Shia Ithnaa Shary, kwa wilaya za Kondoa na Chemba, Shekh Abdullatwifu Swaleh, kwa kushirikia na Taasisi ya World Propagation and Humanitarian Service (WIPAHS), ikiwa ni sehemu ya kusherehekea sikukuu ya Eid El Fitr.

Vifaa vilivyopokelewa kwa ajili ya hospitali hiyo ni pamoja na vitanda kumi na vifaa vya usafi, ambavyo vilikabidhiwa kwa wagonjwa wanaolazwa.

Mganga mfawidhi huyo alisema taasisi, mashirika ya dini na watu binafsi wana nafasi kubwa ya kuhakikisha wanatoa michango yao kwa serikali ili kutatua changamoto wanazokabiliana nazo.

"Kama taasisi, mashirika na watu binafsi wanavyowekeza ikiwapo majengo ya hospitali, shule binafsi, pia wanaweza kuwekeza kwa upande wa serikali na ikafaidika na misaada hiyo muhimu kama hivi vitanda na vifaa vya kufanyia usafi vilivyotolewa hapa," alisema.

"Toka nimefika wilayani hapa Kondoa nina miaka mingi lakini sijawahi kupokea msaada kama huu kwa ajili ya mahitaji ya hospitali hii, kwa maana hii niseme asante sana na vitanda hivi vitatumika kwa wagonjwa na wauguzi waliopo zamu nyakati za usiku," alisisitiza.

Shekh Abdullatwifu Swaleh alisema wataendelea kusaidia jamii yenye uhitaji bila kujali mahusiano yoyote yale ikiwamo dini, kabila wala rangi.

Aliziomba taasisi, mashirika, watu binafsi na madhehebu ya dini kuangalia kwa jicho la huruma watu ambao katika maisha yao ya kila siku wamekuwa wakiyaona ni magumu.

**"Toka nimefika wilayani hapa Kondoa nina miaka mingi lakini sijawahi kupokea msaada kama huu kwa ajili ya mahitaji ya hospitali hii, kwa maana hii niseme asante sana na vitanda hivi vitatumika kwa wagonjwa na wauguzi waliopo zamu nyakati za usiku," alisisitiza.**

# Wakurugenzi waagizwa maji shuleni

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

NAIBU Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Gerald Mweli, amewataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kuhakikisha shule zinakuwa na maji ya kutosha ili kuwakinga wanafunzi dhidi ya maambukizo ya virusi vya corona.

Aidha, amewatoa hofu, wazazi na walezi wa wanafunzi kuwa serikali inaweka mikakati ya kuhakikisha wanafunzi wanakuwa salama wakiwa shuleni katika kipindi hiki cha janga la corona.

Mweli aliyasema hayo jana jijini Dodoma baada ya kutembelea shule za sekondari za serikali na binafsi ili kuangalia zilivyojiandaa kuwapokea wanafunzi wa kidato cha sita na hatua zilizochukuliwa kudhibiti maambukizo ya corona.

Alisema wakurugenzi wanatakiwa kusimamia kwa karibu, na kuhakikisha shule zinakuwa na huduma ya maji na zinachukua tahadhari za ziada katika kuwakinga wanafunzi kwa kufuata mwongozo wa Wizara ya Afya.

"Wakurugenzi mhakikishe idara ya afya na elimu katika halmashauri zenu zinafanya kazi kwa karibu kwa kuchukua tahadhari na hatua za haraka endapo kutatokea tatizo kwa wanafunzi," alisema.

Pia, Mweli aliwataka wakuu wa shule kuhakikisha wanawajenga wanafunzi kisaikolojia na kuwaondolea hofu ili wazingatie masomo yao.

"Mwanafunzi akitoka nyumbani kwa mzazi na kuja shuleni, wajibu wa kumwangalia ni wenu ninyi walimu, hivyo muwajenge kisaikolojia na kuwaondoa hofu kwa kuwaambia kuwa ukichukua tahadhari kulingana na miongozo utakuwa salama," alisema.

Vilevile Mweli aliwatoa hofu wazazi na walezi kuwa serikali inachukua tahadhari zote zinazotolewa na wizara ya afya ili kuhakikisha wanafunzi wanakuwa salama muda wote wawapo shuleni.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Maduka Kessy, alisema mkoa umejipanga kuwapokea wageni na kuhakikisha Dodoma inakuwa salama na hakuna maambukizo mapya.

"Dodoma ina vyuo vikuu na vya kati pamoja na shule za sekondari 17, hivyo tunajua tutakuwa na ugeni wa watu wengi baada ya vyuo na wanafunzi wa kidato cha sita kurejea...tumeweka mikakati ya kuhakikisha Dodoma haipati maambukizo mapya," alisema Kessy.

Alisema wanakwenda kufanya ukaguzi katika shule kuhakikisha maji yapo na misaada ambayo mkoa umepata wa vifaa vya kujikinga na corona kama vitakasa mikono, sabuni na vifaa vya kunawia vinaelekezwa kwenye shule.

"Mpaka jana Dodoma ilikuwa na wagonjwa wawili ambao muda wowote wataruhusiwa kwa sababu wanaendelea vizuri, hivyo tunataka kuhakikisha hatupati maambukizo mapya. Pia tumepanga kuwasambaza wahudumu wa afya katika shule ili kuwa karibu na wanafunzi," alifafanua Kessy.

Mkuu wa Shule Salesian Seminary Dodoma, Father Oscar Rutechungura, alisema kwa kutumia chuo cha ufundi cha Don Bosco, wamejiandaa kwa kutengeneza vifaa vya kunawia mikono na barakoa ambazo watakuwa wakiwapa wanafunzi ambao watakuwa na mafua au kikohozi.



Meneja Kilimo wa Tanzania Breweries Ltd (TBL), Joel Msechu (kushoto), akikagua aina ya mtama mweupe kwa wakulima wa kijiji cha Bumbuta, wilayani Kondoa, mkoani Dodoma juzi, akiwa katika ziara ya kuangalia aina ya mtama inayofaa kwa ajili ya kuzalisha vinywaji aina ya bia kwenye viwanda vya kampuni hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Jiji latekeleza falsafa ya JPM kuwajali machinga

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, amesema halmashauri hiyo inaendelea kutekeleza falsafa ya Rais John Magufuli ya kuwajali na kuwapa kipaumbele wafanyabiashara wadogo (machinga).

Kunambi alisema ili kila Mtanzania ashiriki kukuza uchumi wa viwanda, ni wajibu wa Halmashauri ya Jiji hilo kuwapa nafasi watu wote ikiwa ni pamoja na mama lishe kwa kuwatengenezea mazingira mazuri ya kufanyia shughuli zao katika kituo kikuu kipya cha mabasi cha mkoa.

Kunambi aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kukamilika kwa utoaji fomu kwa ajili ya maeneo ya biashara katika kituo kikuu cha mabasi cha Dodoma na soko kuu la Job Ndugai.

Kunambi alisema halmashauri yake inatekeleza dhamira ya Rais Magufuli ya kuwatengenezea mazingira rafiki wamachinga.

"Niseme wazi kuwa machinga ni sehemu ya hii stendi, hivyo kama mnavyoona eneo hili katika kituo kikuu cha mabasi cha Dodoma tumetenga maeneo mawili maalum kwa ajili ya machinga," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema halmashauri yake imeenda mbali zaidi na kuwafikiria mamalishe wanaofanya shughuli zao katika stendi ya mabasi ya Nanenane.

"Wapo mamalishe wanaofanya shughuli zao katika stendi ya sasa ya Nanenane, baada ya stendi hiyo kuhama na kuanza kutumika kituo kikuu cha mabasi cha Dodoma, tutahama nao," alisema Kunambi.

Alisema amemwelekeza mkuu wa idara ya maendeleo ya jamii na vijana kuwaratibu vizuri ili waweze kupatiwa mikopo ya asilimia 10 ya halmashauri kwa ajili ya kuboresha shughuli zao.

Akizungumzia mchakato wa wafanyabiashara walioomba nafasi za kufanya biashara katika kituo kikuu cha mabasi na Soko Kuu la Job Ndugai, alisema kuwa orodha ya wafanyabiashara waliofaulu kupata nafasi za kufanyabiashara itatolewa hadharani.

"Kuanzia leo wafanyabiashara wote waliofaulu kupata nafasi za biashara wafuatilie majina yao katika tovuti ya Halmashauri ya Jiji na katika mbao za matangazo ili waweze kuchukua fomu za masharti ya upangaji katika maeneo ya biashara na taratibu za kulipia ada," alisema Kunambi.

Mkurugenzi huyo aliyataja maeneo ambayo yamebaki bila kupata wapangaji ni bucha mbili na sehemu za kupokelea mizigo 11, katika Soko Kuu la Job Ndugai na maeneo ya maduka tisa ya mita za mraba 36 pamoja na vizimba 33 vya biashara. Alisema maeneo hayo yatatangazwa upya ili wafanyabiashara waweze kuomba ili kupangishwa.

Aidha, alimshukuru Rais Magufuli kwa kutoa fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo katika Jiji la Dodoma zaidi ya Sh. trilioni moja.

Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi Dodoma umegharimu kiasi cha Sh. bilioni 24, na soko kuu la Job Ndugai umegharimu Sh. bilioni 14.





# Wafanya ibada kumshukuru Mungu kunusuru corona

**Na Grace Mwakalinga, CHUNYA**

WAUMINI wa madhehebu mbalimbali ya Kikristo katika Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya, wakiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Maryprisca Mahundi, wamefanya ibada ya kumshukuru Mungu kwa kulinusuru taifa na janga la ugonjwa wa Covid-19.

Mahundi aliyeongoza ibada hiyo ya shukrani mwishoni mwa wiki katika Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Chunya, alisema uamuzi wa Rais Dk. John Magufuli kuiombea nchi ni darasa kwa mataifa mengine.

Alisema Rais Magufuli amekuwa kiunganishi kati ya wananchi na Mungu kwa kupitia maombi na kwamba uamuzi huo umelisaidia taifa kuondokana na hofu ya ugonjwa huo.

"Hatuna budi kumpongeza Rais Dk. Magufuli kwa namna alivyoongoza vyema mapambano dhidi ya ugonjwa huo hakika amekuwa darasa kwa nchi nyingi duniani, wako baadhi walifikiri vita hii tutashindwa, lakini kupitia mtumishi wa Mungu Dk. Magufuli tumeishinda na huu ni wakati wa kurudisha shukrani kwa mola alisema," Mahundi.

Aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo kwa kufuata ushauri na maelekezo ya wataalamu, kwa kuwa bado corona ipo na inaua, ingawa kwa sasa maambukizo yamepungua nchini kwa kiwango kikubwa.

Mwinjilisti Asifiwe Naiman, alisema licha ya kuwapo kwa utabiri uliofanywa na wataalamu wa nje ya nchi kuwa Tanzania itapata maafa makubwa kwa ugonjwa wa corona, lakini Mungu amewalinda akimtumia Rais Dk. Magufuli kuwaongoza vyema Watanzania kuvuka janga hilo.

Alisema taifa limeona ukuu wa Mungu kwa kuwanusuru na janga hilo licha ya baadhi ya watu hususani wanaharakati kudai hatua zinazochukuliwa hazina mashiko.

**"Hatuna budi kumpongeza Rais Dk. Magufuli kwa namna alivyoongoza vyema mapambano dhidi ya ugonjwa huo hakika amekuwa darasa kwa nchi nyingi duniani, wako baadhi walifikiri vita hii tutashindwa, lakini kupitia mtumishi wa Mungu Dk. Magufuli tumeishinda na huu ni wakati wa kurudisha shukrani kwa mola alisema," Mahundi.**

# Vijiji 33 kuondolewa Hifadhi ya Ruaha

**Na Grace Mwakalinga, MBARALI**

JUKWAA la wakulima na wafugaji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, limesema agizo la Rais Dk. John Magufuli la kutaka vijiji vilivyomo ndani ya mipaka ya hifadhi za taifa viondolewe, bado halijatekelezwa kikamilifu.

Jukwaa hilo limesema hadi sasa halijaona kijiji hata kimoja ambacho kimeondolewa kisheria ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na kurejeshwa kwa wananchi.

Hayo yalisemwa jana na jukwaa hilo ambalo lilikutana katika Mji Mdogo wa Rujewa kwa lengo la kujadili masuala mbalimbali, ikiwamo utekelezaji wa agizo la Rais Magufuli la kuviondoa vijiji ambavyo vilionekana vipo ndani ya hifadhi za taifa nchini.

Katibu wa Jukwaa hilo wilayani humo, Christopher Uhagile, alisema Baraza la Mawaziri ambalo lilifika wilayani Mbarali lilikubaliana vijiji zaidi ya 900 vinaondolewa kwenye hifadhi na kukabidhiwa wananchi.

Alisema hadi sasa hakuna hatua zozote zilizofanyika na kuvirudisha vijiji hivyo kwa wananchi na hawajui lini suala hilo litatekelezwa licha ya kupewa ahadi.

Uhagile alisema jukwaa linasikitishwa na hotuba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, aliyoitoa bungeni wakati akiwasilisha bajeti ya wizara yake na kueleza kuwa wametekeleza agizo la Rais Magufuli kuviondoa ndani ya hifadhi za taifa vijiji 920 wakati wao hawajaona mchakato wowote wa kisheria wa utekelezaji wa suala hilo.

"Sisi jukwaa tunasikitishwa na hotuba ya Waziri Lukuvi, kwamba vijiji 920 kuviondoa kwenye hifadhi, kiukweli hatujaona mchakato wowote wa kisheria, tunafahamu suala hili liko kwenye vyombo vya maamuzi ndio maana ziliundwa tume, lakini tunachohitaji ahadi itekelezwa," alisema Uhagile.

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa Jukwaa hilo Wilaya ya Mbarali, Matagili Mbigili, alisema migogoro ya ardhi baina ya wakulima na wafugaji haiwezi kumalizika ikiwa mipaka inayotenganisha maeneo ya wananchi na hifadhi za taifa haitawekwa na kutambulika kisheria na ikaonekana kwa uwazi na watu wote.

Walisema Mbunge wa Mbarali anayo nafasi ya kulishughulikia suala hilo, kwa kuhakikisha analifikisha bungeni kujadiliwa ili vijiji hivyo ambavyo viko kwenye hifadhi virudishwe kwa wananchi kuliko ilivyo sasa.

Jumla ya vijiji 33, wilayani Mbarali vinatakiwa kuondolewa ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Magufuli la kuviondoa vijiji zaidi ya 900 vilivyo ndani ya hifadhi mbalimbali za taifa nchi nzima.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila (kushoto), akizungumza na viongozi mbalimbali wa dini, mila na wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya mkoa huo, jana, wakati wa kikao maalumu kilichojadili mambo mbalimbali ikiwamo mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Maeneo yaliyovamiwa kujengwa taasisi umma

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ameagiza wakurugenzi wa halmashauri zote mkoani humo, kuchukua maeneo yote ya ardhi ambayo yamevamiwa ama kutapeliwa na watu kinyume cha utaratibu na kuyatumia kujenga taasisi za umma kama vile shule, vituo vya polisi au zahanati ambazo zitakuwa na manufaa kwa wananchi wote.

Chalamila alitoa agizo juzi, wakati akikagua ujenzi wa shule mpya ya msingi yenye mchepuo wa Kiingereza ambayo inajengwa na Jeshi la Kujenga Taifa chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Jiji la Mbeya.


Alisema wanaendelea kuwabaini matapeli wanaowaibia wananchi ardhi zao na hata serikali na kwamba wamebuni mbinu mpya ambayo yeyote atakayebainika itataifishwa kwa kujenga taasisi mbalimbali za umma zikiwamo shule.

"Mtindo huo utasaidia kupunguza wimbi la matapeli pamoja na madalali wasio waaminifu, naagiza viongozi wote wa wilaya na halmashauri za mkoa huo kutumia njia hiyo kuongeza na kusogeza huduma za kijamii karibu na wananchi," alisema Chalamila.

Akisoma taarifa ya ujenzi wa shule hiyo, Ofisa Uchumi wa Halmashauri ya Jiji, Saad Mtambule, alisema kazi ya ujenzi wa shule hiyo inafanywa na Jeshi la Kujenga Taifa, kikosi namba 844 Itende JKT kwa gharama ya zaidi ya Sh. milioni 460.

Kaimu Kamanda wa Kikosi cha 844 KJ Itende JKT, Luteni Kanali Juma Mlay, alisema kuwa kazi hiyo itakamilika ndani ya mwezi mmoja ujao.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya jiji hilo, Kamishna Msaidizi wa Polisi, James Kasusura, alisema shule hiyo ilipewa jina la Magufuli English Medium Primary School kwa lengo la kuthamini na kutambua mchango wa Rais Magufuli katika kukuza elimu nchini.





# Walimu 667 waajiriwa, wengine 435 mbioni

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imesema jumla ya walimu 667 wameajiriwa na kupangiwa vituo vya kazi, huku walimu wengine 435 wakiwa katika hatua za mwisho za taratibu za ajira.

Waziri wa wizara hiyo, Riziki Pembe, aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akitoa ufafanuzi kuhusu suala la ajira kwa walimu pamoja na kupunguza tatizo la uhaba wa walimu wa masomo ya sayansi.

Alisema walimu waliopo katika taratibu za kukamilisha ajira watapelekwa katika maeneo yenye upungufu ikiwamo vijijini katika majimbo ya wawakilishi.

Alieleza kuwa katika ajira kipaumbele kimetolewa kwa walimu ambao walikuwa wakijitolea zaidi ya miaka mitano hadi sita katika maeneo ya vijijini Unguja na Pemba.

"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika mwaka wa fedha 2020-2021 kipaumbele chake kikubwa ni kulivalia njuga tatizo la uhaba wa walimu zaidi vijijini pamoja na masomo ya sayansi... tumeajiri walimu wa kutosha na sasa tunataka kuona mafanikio katika sekta ya elimu ikiwamo kiwango cha ufaulu mitihani ya taifa," alisema.

Pembe alisema katika suala la ajira kilio cha muda mrefu cha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kuhusu uhaba wa walimu katika majimbo yao kimezingatiwa na kusikilizwa.

Hata hivyo, aliwataka walimu wote walioajiriwa kuzingatia masharti ya kazi ikiwamo kufanya kazi na kuacha visingizio baada ya muda mfupi kuomba uhamisho.

"Lipo tatizo la walimu wanaopangiwa kazi vijijini baada ya muda mfupi huomba uhamisho na kutaka kurudi mjini kwa kisingizio cha kuwafuata waume zao.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Haroun Ali Suleiman, alisema ajira za walimu ni sehemu ya utekelezaji wa mikakati ya Rais wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, kuona tatizo la uhaba wa walimu katika shule za vijijini linaondoka moja kwa moja.

"Tumepewa kibali cha kuajiri watumishi mbalimbali, ambapo kipaumbele cha kwanza ni walimu kwa lengo la kuona hakuna uhaba wa kada hiyo," alisema.

**"Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika mwaka wa fedha 2020-2021 kipaumbele chake kikubwa ni kulivalia njuga tatizo la uhaba wa walimu zaidi vijijini pamoja na masomo ya sayansi...tumeajiri walimu wa kutosha na sasa tunataka kuona mafanikio katika sekta ya elimu ikiwamo kiwango cha ufaulu mitihani ya taifa," alisema.**

# Kibano wanunuzi binafsi wa karafuu kwa wakulima

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SHIRIKA la Taifa la Biashara (ZSTC), limesema ni makosa kwa mujibu wa Sheria ya Karafuu Namba11 ya Mwaka 2011 kwa mtu binafsi ikiwamo wafanyabiashara kununua zao hilo kutoka kwa wakulima.

Mkurugenzi Mwendeshaji wa ZSTC, Dk. Said Seif Mzee, alisema hayo kufuatia kujitokeza kwa baadhi ya wafanyabiashara kununua karafuu kutoka kwa wakulima, huku wengine wakipita sehemu za vijijini na kujifanya ni wakala wa shirika hilo.

Alisema shirika ndilo lenye mamlaka kwa mujibu wa sheria ya mwaka 2011 kununua karafuu kutoka kwa wakulima tangu mwaka 1968, ambapo shirika hilo lilianzishwa rasmi kwa mujibu wa sheria.

Alisema watu wanaofanya hivyo wajue wanakwenda kinyume cha sheria na watakapobainika watachukuliwa hatua za kisheria na kuingia katika makosa ya uhujumu uchumi na la kufanya magendo.

"Napenda kuwajulisha wananchi kwamba shirika la ndilo lenye mamlaka na jukumu la kununua karafuu zote kutoka kwa wakulima kwa mujibu wa Sheria Namba11 ya mwaka 2011 na halijateua wakala wa kufanya kazi hiyo," alisema.

Kwa mujibu wa Sheria ya Karafuu ya Mwaka 2011 pamoja na marekebisho yake, mtu atakayetiwa hatiani akijishughulisha na kununua karafuu atalipa faini Sh. milioni 10 au kwenda jela miaka isiyopungua mitano.

Dk. Mzee alisema ZSTC inaendelea na kazi ya kununua karafuu kutoka kwa wakulima ambapo jumla ya tani 4,000 zenye thamani ya Sh. bilioni 62 zimenunuliwa katika msimu uliomalizika mwezi uliopita.

Alisema si kweli kwamba shirika limeshindwa kununua karafuu kutoka kwa wakulima na ndiyo sababu baadhi ya watu hutumia kisingizio cha kununua karafuu hizo kwa njia ya ulanguzi.

Alieleza kuwa vipo jumla ya vituo vya kununulia karafuu 33 ambavyo vinafanya kazi, huku wakulima wengine wakivitumia kuuza karafuu zao.

"Hatujasitisha ununuzi wa karafuu kutoka kwa wakulima, vituo vyetu 33 vinafanya kazi Unguja na Pemba kununua karafuu za wakulima, kwa hiyo hawana sababu za kuuza kwa walanguzi," alisema.

Shirika hilo linaendelea kununua karafuu kutoka kwa wakulima kilo moja kwa Sh. 14,000 licha ya bei ya zao hilo kushuka katika soko la dunia.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma (katikati), akijadiliana jambo na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, Haji Omar Kheri (kulia) na Naibu Waziri wa Elimu, Simai Muhamed Said nje ya ukumbi wa Baraza la Wawakilishi, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Pemba wapewa tano mapambano corona

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WANANCHI wa kisiwa cha Pemba wamepongezwa kwa kufanikiwa kupambana kikamilifu na ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona kwa kupunguza maambukizo yake kwa kiwango kikubwa.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa), Shamata Khamis Shaame, wakati akipokea vifaa vya kupambana na ugonjwa wa Covid-19 kwa hospitali tatu za kisiwa cha Pemba.

Alisema mafanikio hayo yamefikiwa kutokana na wananchi kutekeleza masharti ya kupambana na ugonjwa huo ikiwamo kuvaa barakoa na kupunguza mikusanyiko, huku watu wanaoingia katika kisiwa hicho kutoka mikoa jirani ya Tanzania Bara na Mombasa nchini Kenya kuchunguzwa afya zao.

"Tumefanikiwa kupunguza maambukizo ya ugonjwa wa Covid-19 kwa sababu wananchi wamekuwa watiifu wakifuata masharti ya ugonjwa huo, ambayo ni kupunguza mikusanyiko isiyokuwa na ulazima," alisema.

Aliipongeza Taasisi ya Milele Foundation kwa kushirikiana na Wazanzibari waliopo nje ya nchi kusaidia vifaa hivyo katika hospitali nne muhimu za kisiwa hicho.

Baadhi ya vifaa vilivyotolewa na taasisi hiyo ni nguo maalum kwa ajili ya watu wanaotoa huduma kwa wagonjwa wa corona, vifaa vya kupima joto la mwili, vitakasa mikono na sabuni.

Mratibu wa Milele Foundation kisiwani Pemba, Abdallah Said, alisema wameamua kutoa vifaa hivyo kwa hospitali nne za kisiwa hicho ikiwa ni sehemu ya kupambana na maambukizo.

Alisema wamefarijika kwa kiasi kikubwa kuona kwamba wananchi wengi wa kisiwa cha Pemba wamehamasika ikiwamo kuvaa barakoa katika maeneo yote ya miji mitatu mikuu ya Chake Chake, Mkoani na Wete.

"Vifaa vilivyotolewa na Taasisi ya Milele Foundation lengo lake kubwa ni kusaidia mapambano dhidi ya ugonjwa wa corona na kuona wananchi wanakuwa salama, huku wakifanya shughuli zao za maendeleo na ujenzi wa taifa," alisema.

Vifaa vilivyotolewa gharama yake ni Sh. milioni 30.

Akipokea vifaa hivyo, Ofisa Mdhamini Wizara ya Afya Pemba, Shadya Shaaban Seif, alisema msaada huo umekuja wakati mwafaka ambapo Wizara ya Afya ipo katika mapambano ya ugonjwa wa Covid-19.

Seif aliwapongeza wananchi wa kisiwa cha Pemba na mikoa yake miwili kwa kufanya juhudi kubwa za kupambana na maambukizo ya ugonjwa wa huo na kupungua kwa kiwango kikubwa.

"Ninachoweza kusema kwa ufupi kwamba tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kisiwa cha Pemba kupambana na ugonjwa wa Covid-19 na kushusha maambukizo yake na kuwafanya wananchi kufanya shughuli zao huku wakiweka tahadhari," alisema.

Aliahidi vifaa hivyo kutumika kwa malengo yaliyokusudiwa ikiwamo vitanda ambavyo vitatumiwa kwa wagonjwa watakaolazwa katika hospitali nne za kisiwa cha Pemba zikiwamo Chake-Chake, Wete pamoja na Hospitali ya Abdallah Mzee.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


*NIPASHE NI JIBU LAKO*

**NJOO UTANGAZE NASI**

**KWA BEI NAFUU SANA**

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676


## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**Malundi Kija Malundi** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SANLG** yenye namba za usajili **T58 BJM.** Injini namba **No. SLJ 57FMJ.**

**Chessis No. *LBRSPJBS0A9013228.**
Hivyo yeyote atakayeiona kadi hiyo atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi kilichopo Mjini Bariadi.

Taarifa ya kupotea kwa kadi hiyo, imetolewa katika kituo cha polisi cha Bariadi kwa namba: BAR/RB/3642/2011.

157491

## KUPOTEA KWA CHETI



**Catherine Jumanne Mavere anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne Kilichotolewa kwa mtahiniwa namba S.0250-0010 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kwa mtihani wa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Wasichana Murigha.**

**Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.**

**Taarifa ya polisi namba RV/RB/4073/2019.**

157490

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**
**SHAURI LA GHARAMA NA.93/2020**
**NATIONAL MICROFINANCE BANK::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::MDAI**
**DHIDI YA**
**VICTOR R.MWASHINGAIRE::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::::MDAIWA**

**YAH : KUITWA SHAURINI**

KWA:
1.VICTOR R.MWASHINGAIRE
Fahamu kwamba National Microfinance Bank amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 26/05/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh.A.Mapunda Mwenyekiti wa Baraza. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au muwakilishi ameruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.
Kumbuka:usipo hudhuria siku hiyo,baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 22/04/2020.

157492

## KUPOTEA KWA KADI

EZEKIA ELIAS TWEVE ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA **SANLG T 780 BKR** ILIYOTOLEWA NA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA.

YEYOTE ATAKAEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

POLISI TAARIFA:
**991081274411141**

157489


***Uza, Chenye***

***Thamani***

***Kubwa Kwa***

***Kutangaza***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Ujerumani kulegeza masharti kukaribiana

**BERLIN,** Ujerumani

UJERUMANI imepanga kulegeza hatua za watu kukaribiana kuanzia Juni 29 ikiwa ni wiki moja kabla ya iliyopangwa hapo awali.

Hatua hiyo ina lenga kuondoa vizuizi vya kusafiri kwa mataifa 31 ya Ulaya kuanzia katikati ya mwezi Juni.

Ripoti hiyo inakuja wakati majimbo ya Ujerumani yanajadiliana na Kansela Angela Merkel (pichani chini), kuhusu namna ya kulegeza vizuwizi vya watu kuzuiwa majumbani mwao hatua iliyoanza kutumika mwezi Machi kwa nia ya kupunguza kusambaa corona.

Mawaziri wakuu wa majimbo 16 ya Ujerumani leo watajaribu kukubaliana na Merkel kuhusu hatua ya kuchukua.

Hatua hiyo ikileta uwiano kuhusu mahitaji ya kuufufua uchumi wa taifa hilo lenye uchumi mkubwa barani Ulaya ambao unakabiliwa na mdororo mkubwa tangu baada ya vita vikuu vya pili vya dunia pamoja na kulinda afya ya jamii.

Gazeti la Bild la Ujerumani limesema kuwa mikusanyiko katika maeneo ya umma haitazidi watu 10, ama ndugu wa familia mbili.

Ujerumani imekuwa na idadi ndogo ya vifo 8,302 licha ya idadi ya juu ya maambukizo. **DW**



# WHO yasitisha majaribio Hydroxychloroquine

**GENEVA,** Uswizi

SHIRIKA la Afya Duniani (WHO), limesitisha majaribio ya dawa ya ugonjwa wa malaria Hydroxychloroquine ambayo yamelenga kuona iwapo inaweza kutibu virusi vya corona.

WHO limeamua kuyasitisha majaribio hayo kutokana na hofu ya usalama wake.

Shirika hilo limesema, vipimo vilivyokuwa vikifanywa katika mataifa kadhaa vimesitishwa kwa muda kama hatua ya kuchukua tahadhari.

Hatua hiyo inajiri baada ya utafiti wa tiba uliofanyika hivi karibuni kusema kwamba dawa hiyo inaweza kuongeza hatari ya mgonjwa kufariki kutokana na virusi hivyo.

Rais Donald Trump alisema kuwa anatumia dawa hiyo kuzuia virusi hivyo.

Rais huyo wa Marekani ameikuza dawa hiyo ya malaria, kinyume na ushauri wa kimatibabu na onyo kutoka kwa maofisa wa afya kwamba inaweza kusababisha tatizo la moyo.

**Hydrochloroquine ni dawa salama ya kutibu ugonjwa wa malaria, baridi yabisi na Lupus, lakini hakuna majaribio yoyote ambayo yamependekeza matumizi yake kutibu corona.**

Kwa mujibu wa Chuo Kikuu cha Johns Hopkins, vifo vilivyotokana na corona vimefikia 98,218.

Wiki iliyopita, utafiti uliofanywa na jarida la tiba duniani Lancet, ulibaini kwamba hakuna faida yoyote kwa kutumia dawa ya Hydroxychloroquine na kwamba unaweza kuongeza idadi ya vifo miongoni mwa wagonjwa wa corona hospitalini.

Hydrochloroquine ni dawa salama ya kutibu ugonjwa wa malaria, baridi yabisi na Lupus, lakini hakuna majaribio yoyote ambayo yamependekeza matumizi yake kutibu corona.

Watafiti wanasema kwamba wagonjwa wa corona hawafai kutumia hydroxychloroquine.

WHO linafanyia majaribio dawa kadhaa kuona iwapo zinaweza kutibu ugonjwa huo mbali na kuripoti kwamba baadhi ya watu binafsi wamekuwa wakitumia dawa hiyo na hivyo basi kujisababishia madhara makubwa.

Jumatatu, maofisa katika shirika hilo la Umoja wa Mataifa walisema kwamba hydroxychloroquine itaondolewa kwa muda katika majaribio hayo kwa muda ili kuruhusu uchunguzi wa usalama wake.

Utafiti huo wa Lancet ulihusisha wagonjwa 96,000 wa virusi vya corona ambapo kati yao 15,000 walipatiwa dawa ya Hydroxychloroquine ama ile inayohusishwa na Chloroquine, pekee ama na dawa ya antibiotic.

Utafiti huo ulibaini kwamba wagonjwa hao walikuwa na hatari kubwa ya kufariki hospitalini na kupatwa na tatizo la moyo ikilinganishwa na wagonjwa wengine wa corona.

Hatari ya mgonjwa anayetumia hydroxychloroquine kufariki ilikuwa asilimia 18, asilimia 16.4 kwa waliotumia Chloroquine na asilimia 9 kwa kundi jingine.

Wale waliotibiwa na hydroxychloroquine au chloroquine kwa mchanganyiko na dawa ya antibiotic walikuwa na hatari ya kubwa zaidi kufariki.

Watafiti hao walionya kwamba Hydroxychloroquine haifai kutumiwa kando na majaribio hayo. **BBC**



Rais mteule wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, ambaye ameshinda kwa asilimia 68.72 ya kura zilizopigwa huku Agathon Rwasa kutoka chama cha upinzani cha (CNL) akipata asilimia 24.19. **PICHA: MTANDAO**

# Rais mteule Burundi afunguka upinzani kwenda kortini

**BUNJUMBURA,** Burundi

MSHINDI wa kiti cha urais nchini Burundi, Evariste Ndayishimiye, amesema ushindi wake ni wa raia wote waliomchagua na wale ambao hawakumchagua.

Akihutubia baada ya kutangazwa mshindi, Ndayishimiye alisema ushindi wake ni wa raia wote waliomchagua na wale ambao hawakumchagua.

"Hivyo, hakuna sababu ya wafuasi wa chama kimoja kuwabugudhi wengine," Alisema.

Pia ameitaka jumuiya ya kimataifa kuunga mkono hatua iliyofikiwa nchini humo.

Kiongozi huyo wa chama cha CNDD-FDD aliyeibuka mshindi uchaguzi wa Jumatano iliyopita alisema uchaguzi huo umedhihirisha kukua kwa umahiri wa kisiasa wa Burundi. Ndayishimiye ameahidi kuwasikiliza raia wote Burundi bila ubaguzi.

"Tumejipa hadhi mbele ya Warundi na dunia, kwa kuionesha kuwa tulipofikia hatufundishwi tena demokrasia bali tunaweza kuwafundisha wengine.

"Hivyo ninaahidi kuwa nitawasikiliza wananchi wote bila ubaguzi ili maoni yao yaweze kulijenga taifa. Naitaka jumuiya ya kimataifa kuiunga mkono hatua hii ya kupendeza tuliyoifikia."

Pia Rais huyo mteule alimshukuru mtangulizi wake Rais Pierre Nkurunziza kwa hatua yake ya kuridhia kuanzisha mchakato huo wa uchaguzi.

Ndayishimiye amewataka wakimbizi kurudi nyumbani ili kuchagia ujenzi wa taifa.

Naye, Kiongozi wa upinzani Burundi, Agathon Rwasa, ambaye amechukua nafasi ya pili katika uchaguzi huo, amesema hatokubaliana na matokeo ya uchaguzi yaliyotangazwa na Tume ya Uchaguzi ya Rwanda (CENI).

Rwasa ameahidi kuyafikisha malalamiko yake kwenye mahakama ya kikatiba na endapo hatotendewa haki basi ataelekea kwenye mahakama ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Tayari tume ya Uchaguzi inakutana na wawakilishi wa vyama vya siasa ili kuwateuwa wabunge 21 kutoka katika jamii ya Watutsi na watatu kutoka Watwa watakaojumuishwa katika Bunge la Taifa ili kuleta usawa wa kikabila. **DW**

# SCALONI AIONA NAMBA YA MARTINEZ BARCA




**MILAN,** Italia

LAUTARO Martinez ataweza kupata namba yake pale Barcelona kama akiondoka Inter Milan, kwa mujibu wa Kocha Mkuu wa Argentina, Lionel Scaloni.

Martinez amekuwa akihusishwa na kuondoka kwa miamba hao wa Serie A, Inter na kutakiwa kule kwa mabingwa wa LaLiga, Barca.

Raia huyo wa Argentina amefunga mabao 16 katika mechi 31 alizocheza kwenye mashindano yote kabla ya msimu huu 2019-20 kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Scaloni alipoulizwa kuhusu majaliwa ya Martinez wakati huu, aliiambia redio La Red: "Kama Lautaro akienda Barcelona, nafikiri kocha mkuu (Quique Setien) ataangalia namna ya kumfanya aanze kwenye kikosi cha kwanza, atakwenda kujitolea na kupata nafasi yake."

"Kumchukua Lautaro nje ya Inter haitakuwa kazi rahisi ... ningependa Lautaro Martinez acheze, kuendeleza kipaji chake," aliongeza Scaloni.

"Lautaro ana kitu kimoja, kwamba anacheza kwa ajili yake na wachezaji wenzake. Atakuwa mshambuliaji bora zaidi kwa siku za usoni."

Martinez alisajiliwa hapo Inter akitokea Racing Club mwaka 2018 na haraka akajiimarisha yeye mwenyewe kuwa mmoja wa washambuliaji bora Ulaya.

Amefunga jumla ya mabao 25, tangu alipojiunga na Inter.

# Werner, Cavani wamulikwa Inter Milan

**MILAN,** Italia

OFISA Mtendaji Mkuu wa Pirelli, Marco Tronchetti anataka Inter Milan iwasajili nyota wa RB Leipzig Timo Werner na mshambuliaji wa Paris Saint-Germain, Edinson Cavani wakati huu ambao Lautaro Martinez anahusishwa na Barcelona.

Mshambuliaji wa Inter, Martinez amekuwa akihusishwa sana na mabingwa wa LaLiga, Barcelona, ambao wameripotiwa kwamba wanamtaka mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina kama mrithi wa muda mrefu wa Luis Suarez.

Kwa mujibu wa ripoti, Inter ya Antonio Conte imeweka pamoja orodha ya wachezaji ambao wanaweza kurithi nafasi yake, akiwamo Werner anayewindwa na Liverpool na Cavani ambaye hivi karibuni atakuwa huru.

Tronchetti – Ofisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Pirelli inayoidhamini jezi ya Inter – amewashauri Nerazzurri kuwachukua Werner na Cavani.

"Kwa mfano, tutataka Inter isajili wachezaji ambao wanatakiwa kuibadilisha timu kama (Christian) Eriksen," alisema Tronchetti akiiambia Gr Parlamento.

"Cavani anaweza kuwa mchezaji mzuri na ana nafasi ya kuipa mafanikio timu kwani yeye ni mchezaji mkubwa na mwenye uwezo.






# *Lacazette kupishana na Lemar msimu ujao*

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imeripotiwa kwamba inaweza kumruhusu, Alexandre Lacazette kwenda Atletico Madrid na wao kumchukua Thomas Lemar.

Janga la corona limesababisha matatizo makubwa ya kiuchumi kwa klabu, jambo ambalo limeathiri soko la wachezaji wakati wa dirisha la uhamisho litakapofunguliwa hivi karibuni. Kutokana na hilo dili nyingi za timu katika maandalizi ya msimu mpya wa 2020-21 zinaweza kuwa za kubadilishana wachezaji baada ya pesa kuwa ngumu.

Arsenal ilihusishwa na mpango wa kumsajili Lemar kwenye dirisha la Januari, mwaka huu na sasa imedaiwa ina mpango wa kubadilishana Mfaransa huyo.

Lemar, ameshindwa kufunga katika mechi 24 alizocheza akiwa Atletico Madrid chini ya Diego Simeone, lakini alikuwa kwenye kiwango bora sana wakati akiwa AS Monaco kabla ya kutimkia Hispania.

Lacazette, wakati huo huo, anaripotiwa anaonekana atakwenda kuwa wa ziada katika kikosi cha Mikel Arteta ambaye amekuja na mipango yake moto ya kufanya mabadiliko kwa washambuliaji wake.

# Neville ahofia wachezaji EPL kushuka viwango

**LONDON,** England

GARY Neville anaamini wachezaji wengi watakuwa wameshuka viwango wakati Ligi Kuu ya Egland itakaporejea tena kumalizia msimu.

Serikali ya Uingereza imewasha taa ya kijani kuruhusu Ligi Kuu ya England kurudi tena baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Baada ya ushauri, timu kubwa ambazo zimeanza mazoezi kwenye viwanja vidogo, watapiga kura leo Jumatano kama waendelee na mazoezi kwenye viwanja vikubwa.

Na nahodha wa zamani wa Manchester United, Neville ana furahi kurudi kwa ligi hiyo, lakini anahisi wachezaji wengi hawatakuwa kwenye viwango vyao, hasa baada ya kiungo wa Chelsea, N'Golo Kante na mshambuliaji wa Watford, Troy Deeney, ambao wamekataa kufanya mazoezi kwa hofu ya corona.

"Nafikiri Klabu zitapiga kura ya kuanza kwa ligi wiki chache zijazo," alisema Neville akinukuliwa na Sky Sports.

"Nadhani kutakuwa na wachezaji ambao hawatakuwa kwenye viwango vyao, yaani watakuwa wameshuka viwango.

"Sidhani kama hili litaisaidi Ligi Kuu ya England, lakini kwa sasa ngoja tusubiri na tuangalie nini kitakachotokea."







# IBRAHIMOVIC AUMIA MAZOEZINI AC MILAN

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic amepata maumivu makubwa wakati akijifua kwenye mazoezi kule Milan Jumatatu.

Mchezaji huyo wa zamani wa Sweden aliumia chini ya kigimbi wakati wa mechi ya mazoezi, kwa mujibu wa Stats Perform News.

Ripoti kutoka nchini Italia, zinadai kwamba anaweza kuwa ameumia hadi kwenye kisigino cha mguu.

Ibrahimovic mwenye umri wa miaka 38, alijiunga na AC Milan kama mchezaji huru Desemba mwaka jana, akaingia mkataba ambao unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Alifunga mabao matatu katika mechi nane za Serie A kabla ya mlipuko wa virusi vya corona ambapo ligi hiyo ilisimamishwa tangu Machi.

Kipindi chake hicho cha pili kucheza kule Milan kinaonekana kama ndio mwisho wa kucheza soka la ushindani kwa Ibrahimovic.

Kocha wa Bologna, Sinisa Mihajlovic hivi karibuni alisema kwamba, baada ya kuzungumza na Ibrahimovic, anamtarajia ataondoka Milan mwishoni mwa msimu.

Baada ya kuanza kucheza soka la ushindani katika klabu ya Malmo, akahamia Ajax, Juventus, Inter na Barcelona.

Kwa mara ya kwanza aliichezea Milan Agosti mwaka 2010 na alidumu kwa miaka miwili kabla ya kwenda Paris Saint-Germain. Alikaa miaka minne ya mafanikio pale PSG baadaye akaenda Manchester United alikokaa kwa misimu miwili. Na akacheza kwa miezi 20 kwenye Ligi Kuu ya Marakeni katika Klabu ya LA Galaxy.

# *Felix aipa pigo Atletico Madrid*

**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Atletico Madrid, Joao Felix, anaweza kuwa nje ya dimba kwa muda baada ya kuumia goti lake la kushoto.

Klabu hiyo ya LaLiga, Atletico imebainisha Jumatatu kwamba, mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa ada iliyoweka rekodi klabuni hapo alifanyiwa vipimo katika Kliniki ya Chuo Kikuu cha Navarra, na ilionyesha kwamba ameumia goti.

Atletico sasa ina matumaini mchezaji huyo kijana anaweza kupona kwa wakati kabla ya La-Liga kuanza tena Juni.

Jumamosi, Waziri Mkuu wa Hispania, Pedro Sanchez alithibitisha kwamba wametoa ruhusa kwa ligi kuendelea, lakini bila watazamaji kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Joao amecheza mechi 28 kwa Atleti katika mashindano yote, huku mshambuliaji huyo wa zamani wa Benfica akifunga mabao sita.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND, LEWANDOWSKI WACHAMBULIWA DIMBANI

●●● Ana kipaji kikubwa, lakini Robert mara zote amekuwa mchezaji wa daraja la juu...

**MUNICH,** Ujerumani

ERLING Haaland bado hawezi kulinganishwa na Robert Lewandowski, kwa mujibu wa kocha Hansi Flick, ingawa kocha huyo mkuu wa Bayern Munich anaamini kwamba nyota huyo wa Borussia Dortmund ana siku nzuri zijazo.

Haaland amepamba vyombo vya habari tangu kuhamia Dortmund Januari akiendelea kuonyesha kiwango cha kuvutia alichoanza nacho nusu ya msimu wa kwanza akiwa kule Salzburg.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 19, amefunga mabao 10 katika mechi 10 za Bundesliga, akiiweka Dortmund kwenye mbio za kuwania taji la Ligi Kuu.

**Kikosi hicho cha kocha, Lucien Favre kimepitwa pointi nne na kipo nafasi ya pili nyuma ya Bayern kabla ya mchezo wa jana Jumanne kwenye dimba la Signal Iduna Park.**

Kiwango cha Haaland kimewagusa wengi na hivyo kufananishwa na straika wa zamani wa Dortmund, Lewandowski, ambaye alifunga bao lake la 41 msimu huu katika mashindano yote, wakati Bayern ilipoibuka na ushindi wa 5-2 dhidi ya Eintracht Frankfurt Jumamosi.

Na bado Flick anaamini ni mapema mno kuwalinganisha wawili hao.

"Ni msimu wa kwanza kwa (Haaland), hivyo kumlinganisha kwa sasa ni mapema sana," alisema Flick akiwaambia waandishi wa habari.

"Robert mara zote amekuwa mchezaji wa daraja la juu katika miaka ya hivi karibuni. Lakini Haaland ana kipaji kikubwa.

"Ni mchezaji kijana, lakini ana nguvu sana mbele ya goli. Yeye huwa anataka tu kumaliza.

"Ana kasi na yuko imara. Na kwa umri wake ana nafasi ya kufanya makubwa zaidi kwa siku za usoni."

## ZISIKUPITE

### DEMBELE KWA MKOPO

KLABU ya Barcelona ipo tayari kusikiliza ofa ya mkopo kwa ajili ya winga wa kimataifa wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 23. ***(Daily Mail)***

### EVERTON YATUA NAPOLI

KLABU ya Everton imewasilisha ombi la pauni milioni 40 ili kumsajili kiungo wa kati wa Napoli, Allan mwenye umri wa miaka 29, lakini klabu hiyo inataka dau la pauni milioni 60 kumuuza raia huyo wa Brazil. ***(Il Mattino)***

### UTD KUMFUNGA HENDERSON

MANCHESTER United itamwongezea mkataba golikipa wa timu ya Taifa ya England, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 23, ili kumruhusu kumaliza msimu wake na klabu ya Sheffield United, huku mkataba wake wa sasa ukitarajiwa kumalizika. ***(Telegraph)***

### COUTINHO BASI TENA

KIUNGO wa kati wa Brazil, Phillipe Coutinho, ambaye anacheza kwa mkopo Bayern Munich, huenda asicheze tena msimu huu, baada ya klabu hiyo kutompa mkataba wa kudumu kutoka Barcelona, na sasa ananyatiwa na Chelsea, Arsenal na Tottenham. ***(Sky Sports)***

### ICARDI KITAELEWEKA PSG

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan na Argentina, Mauro Icardi mwenye umri wa miaka 27, anakaribia kuhamia moja kwa moja katika klabu ya Paris St-Germain kwa dau la pauni milioni 54. ***(ESPN)***

### PSG YAMFUATA AUBAMEYANG

KLABU ya Paris St-Germain inafanya mazungumzo na Arsenal katika jaribio la kumsajili mashambuliaji wa klabu hiyo, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 30, kwa pauni milioni 34. ***(Todofichajes)***

### SANE ATAFUTIWA MRITHI CITY

KLABU ya Manchester City imamnyatia winga wa Bayer Leverkusen, Leon Bailey mwenye umri wa miaka 22, raia wa Jamaica, kama mrithi wa Leroy Sane. ***(Mail)***

### MADRID YAMTAKA DE BEEK

REAL Madrid inapanga kutuma ofa ya kumsajili, Donny van de Beek kutoka Ajax, huku Manchester United pia ikionyesha nia ya kumtaka kiungo huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Le10 Sport)***

### CHELSEA WAMTAKA JESUS

WINGA wa Porto na timu ya Taifa ya Mexico, Jesus "Tecatito" mwenye umri wa miaka 27, anawaniwa na Chelsea kama wakishindwa kumsajili nyota wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 20. ***(Star)***

### SPURS, SOUTHAMPTON MEZANI

KLABU ya Tottenham Hotspur inaweza kumtoa mlinzi wake, Kyle Walker-Peters mwenye umri wa miaka 23, kama sehemu ya kubadilishana na kiungo wa Southampton na Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 24, kipindi cha majira ya joto. ***(Football Insider)***

### BOURNEMOUTH NUSURA IUZWE

MMILIKI wa Klabu ya Bournemouth, Maxim Demin alikaribia kuiuza klabu hiyo kwa mfanyabiashara wa Saudi Arabia Januari, kabla ya makubaliano hayo kugonga mwamba kuhusiana na thamani yake. ***(90min)***

# Simba kupeleka kombe lao Chato

**Na Faustine Feliciane**

HUKU Ligi Kuu ikitarajiwa kurejea tena kuanzia Juni Mosi, mwaka huu baada ya kusimama kwa muda kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, Simba imeanza mipango ya kutembeza kombe kwa mashabiki wao, baada ya kutangaza kulipeleka wilayani Chato anapotoka Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano cha klabu hiyo, Hajji Manara, jana aliweka wazi kuwa, hawana shaka na ubingwa msimu huu, hivyo wanasubiri wakati ufike tu ili kulikabidhiwa.

"Ni suala la wakati tu, ubingwa tutauchukua na kama itampendeza Rais Magufuli tumepanga kulipeleka kwake kwa sababu litakuwa letu moja kwa moja kwa kutwaa misimu mitatu mfululizo," alisema Manara.

Alisema hawana mashaka na ubingwa kwa sababu wana kikosi imara na kipana huku kila mchezaji akiwa na kiwango kikubwa.

"Wapo wachezaji ambao wapo nje ya Tanzania, lakini tayari taratibu zinafanyika kuweza kurudi, wapo Meddie Kagere (pichanichini), Francis Kahata na [Sharaf] Shaibou ambao walikuwa nchini kwao.

Hadi Ligi Kuu inasimama Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa virusi vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa COVID-19, Simba ipo kileleni ikiwa na pointi 71, ikifuatiwa na Azam FC yenye ama 54 baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 28, Yanga iliyopo mchezo mmoja nyuma ina pointi 51 katika nafasi ya tatu.



# MEXIME APONGEZA LIGI KUU KITUO KIMOJA

**Na Saada Akida**

WAKATI baadhi ya makocha wakionyesha kutoridhishwa na uamuzi uliotolewa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi (TPLB) na wizara husika ya michezo kuhusu Ligi Kuu Bara kuchezwa katika kituo kimoja, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Mecky Mexime, amesema kwake haoni tatizo na kwamba anaunga mkono kwa asilimia zote.

Ikumbukwe baada ya serikali kutangaza michezo kurejea siku yoyote kuanzia Juni Mosi, mwaka huu, imepangwa Ligi Kuu Bara kuchezwa Uwanja wa Taifa, Uhuru na Azam Complex jijini Dar es Salaam wakati Ligi Daraja la Kwanza na la Pili itachezwa jijini Mwanza katika Uwanja wa CCM Kirumba na Nyamagana.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam jana, Mexime alisema ameona jambo la busara kwa uamuzi ya kuchezwa kituo kimoja kutokana na hali ya janga la corona linaloendelea duniani.

**Alisema kwa upande wake popote wakipangiwa kwenda kucheza, watacheza kwa sababu kikosi chake kimejipanga ili kumalizia michezo iliyobaki.**

"Popote kule tungepangiwa kwangu hakuna tatizo, kikubwa ni kufanya maandalizi mazuri, hivyo tayari kikosi changu tunaenda kujiandaa kupambana kwa ajili ya kurejea kwenye ligi," alisema Mexime ambaye amekuwa akiwindwa na Yanga kwa nyakati tofauti.

Alisema wachezaji wake na watendaji wengine wa benchi la ufundi walianza safari jana kuelekea Kagera kwa ajili ya maandalizi ya kurejea kwenye ligi hiyo ambayo bado TFF haijatangaza tarehe rasmi ya kuanza licha ya serikali kutoa baraka zake kuwa inaweza kuanza kuanzia Juni Mosi.

"Tuombe Mungu tufike salama Kagera, tutajua tunaanza na utaratibu wa kupimana na kufuata maelekezo ya serikali juu ya kujikinga na ugonjwa huu," alisema.

Hadi Ligi Kuu inasimama Machi 17, mwaka huu, Kagera Sugar ilikuwa katika nafasi ya nane ikiwa na alama 41 baada ya kushuka dimbani mara 29.

**POPOTE TU...**



Kocha wa Kagera Sugar, Mecky Mexime, ambaye ameeleza yupo tayari kuiongoza timu yake kucheza popote, baada ya Shirikisho la Soka nchini (TFF) kutangaza Ligi Kuu kuchezwa Kituo cha Dar es Salaam pekee kwenye Uwanja wa Taifa, Uhuru na Azam Complex. **PICHA: MAKTABA**

# *Hitimana ashusha hofu Namungo*

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Mnyarwanda Thierry Hitimana, ametuliza hofu kwa uongozi wa klabu hiyo baada ya kurejea jana akitokea kwao Rwanda, alipokuwa amekwama kutokana na mipaka ya nchi kufungwa.

Hitimana alirejea kwao baada ya Ligi Kuu Bara kusimama tangu Machi 17, mwaka huu kutokana na mlipuko wa maambukizo ya virusi vya corona, lakini Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli,ameruhusu ligi irejee siku yoyote kuanzia Juni Mosi baada ya kuridhishwa na kupungua kwa maambukizo nchini na kasi ya wagonjwa walioambukizwa kupona.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mwenyekiti wa Namungo, Hassan Zidadu, alisema licha ya Tanzania kufungua viwanja vya ndege, bado kwao ulikuwa mtihani mkubwa kwa sababu ya kocha wao huyo kukwama kuja nchini kutokana Rwanda kutofungua mipaka.

Lakini jana Hitimana alirejea baada ya kupatiwa kibali maalum na serikali ya Rwanda, kutokana na nchi hiyo kuwa bado kwenye karantini ya kukabiliana na ugonjwa wa COVID-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

Akizungumza kutoka Rwanda, mtangazaji na mchambuzi wa masuala ya michezo nchini huko, Clever Kazungu alisema kocha huyo pamoja na mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, walipata kibali maalum kila mmoja, kwa sababu walitoa taarifa kuwa wanataka kurejea kazini kwao.

"Serikali ya Rwanda mpaka sasa bado imefunga mipaka yake, hata kutoka hapa kwenda nchi jirani kama DR Congo na Burundi ambapo ni rahisi zaidi kwa watu kusafiri bado kwa sasa wamezuia, lakini Kagere na Hitimana wao wamepewa vibali maalum kwa sababu kila mmoja aliomba kuwa anataka kurejea kazini kwake nje ya nchi," alisema mtangazaji huyo.

Alisema imekuwa rahisi zaidi kwa wachezaji hao kwa sababu baadhi ya viongozi wa Rwanda ni mashabiki wakubwa na michezo hususan mpira wa miguu na wanafahamiana na wachezaji, hivyo mara nyingi huwasaidia sana na kwao ni rahisi kuwasiliana na kumaliza jambo hilo kwa wakati.

Michezo
Jumatano Mei 27, 2020
Nipashe



Haaland, Lewandowski wachambuliwa dimbani UKURASA 22

NIMEREJEA...



Mshambuliaji wa Simba, Meddie Kagere, ambaye amerejea nchini jana akitokea kwao Rwanda, tayari kujiunga na kikosi cha timu hiyo kujiandaa na Ligi Kuu Bara inayotarajiwa kuanza wakati wowote kuanzia Juni Mosi, mwaka huu. **PICHA: MTANDAO**

## Wazawa 7 wenye harufu ya Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

TAYARI Kocha Mkuu wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael amekiri msimu huu ni vigumu timu hiyo kutwaa ubingwa, hivyo malengo yao makubwa mbali na kuwania Kombe la FA, ili kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa, ni kukijenga kikosi chake kwa ajili ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu msimu ujao.

Kukata huko tamaa kwa Eymael, kunatokana na Simba kuongoza kwa pointi 20 zaidi ya Yanga ambayo ipo nafasi ya tatu ikiwa na alama 51 baada ya kushuka dimbani mara 27.

Ingawa msimu haujamalizika ili kutoa nafasi ya kufunguliwa kwa dirisha jipya la usajili, tayari majina ya wachezaji walioonyesha uwezo mkubwa ndani na nje ya nchi, wameanza kuhusishwa na miamba hiyo ya mtaa wa Twinga na Jangwani, Yanga. Licha ya Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli kwa nyakati tofauti kueleza hakuna mchezaji ambaye klabu hiyo imeanza kufanya naye mazungumzo kwa sasa kwa kuwa dirisha bado halijafunguliwa, tayari kuna wazawa saba ambao miongoni mwao wanaweza kusajiliwa na klabu hiyo.

Wachezaji ambao hadi sasa wanahusishwa na klabu hiyo ni mshambuliaji Relliats Lusajo na kiungo Lukas Kikoti wote kutoka Namungo FC. Beki wa Coastal Union, Bakari Mwamnyeto na pacha wake Ibrahim Ame, Baraka Majogoro na Yassin Mohamed wa Polisi Tanzania pamoja na mshambuliaji wa Kagera Sugar, Yusuph Mhilu.

Mtihani mkubwa wa kusajiliwa ama kutosajiliwa kwa wachezaji hao ni wazi utakuwa kiwango watakachoonyeshwa kwa kila mchezaji katika mechi zilizosalia kabla ya msimu kumalizika wakati huu Ligi Kuu ikitarajiwa kuchezwa katika kituo cha Dar es Salaam kwenye Uwanja wa Taifa, Uhuru na Azam Complex, lengo likiwa ni kupunguza kasi ya maambukizo ya virusi vya corona.

# KAGERE ATUA BONGO KWA KIBALI MAALUM

**Na Adam Fungamwango**

### ●●● Sven sasa ahesabu mechi nne za ubingwa Simba huku akiahidi wanaosugua benchi...

STRAIKA hatari wa Simba, Meddie Kagere ametua nchini akitokea kwao Rwanda baada ya kupata kibali maalum cha kumruhusu kutoka nchini humo kutokana na nchi hiyo bado iko kwenye karantini ya kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19 unaosababishwa na virusi vya corona.

**Kagere alitua jana majira ya saa kumi kasorobo kwa ndege ya Shirikika la Ndege la Tanzania ikitokea Mwanza ambako alifika jijini humo juzi, baada ya kuvuka mpaka.**

Mtandao rasmi wa Simba ulionyesha mubashara tukio zima la mchezaji huyo anayeongoza kwa kufumania nyavu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwasili na kupokelewa na kiongozi mmoja wa klabu hiyo.

Kutua kwa straika huyo kumeshusha presha ya wanachama na mashabiki wa klabu hiyo ambao hawakuwa na uhakika wa kurejea kwake hivi karibuni baada ya serikali ya Rwanda kufunga mipaka yake kutokana na virusi vya corona.

Awali, mtangazaji na mchambuzi wa masuala ya michezo nchini Rwanda, Clever Kazungu aliliambia Nipashe kuwa, Kagere na Kocha Mkuu wa Namungo FC, Thiery Hitimana wote raia wa huko, walipata kibali maalum kila mmoja, kwa sababu walitoa taarifa kuwa wanataka kurejea kazini kwao.

"Serikali ya Rwanda mpaka sasa bado imefunga mipaka yake, hata kutoka hapa kwenda nchi jirani kama DR Congo na Burundi ambapo ni rahisi zaidi kwa watu kusafiri, lakini kwa sasa wamezuia, lakini Kagere na Hitimana wao wamepewa vibali maalum kwa sababu kila mmoja aliomba kuwa anataka kurejea kazini kwake nje ya nchi," alisema mtangazaji huyo.

Alisema imekuwa rahisi zaidi kwa wachezaji hao kwa sababu baadhi ya viongozi wa Rwanda ni mashabiki wakubwa wa michezo hususan mpira wa miguu na wanafahamiana na wachezaji, hivyo mara nyingi huwasaidia sana na kwao ni rahisi kuwasiliana na kumaliza jambo hilo kwa wakati.

Katika hatua nyingine, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck amesema kimahesabu wanahitaji pointi 12 pekee sawa na michezo minne ili kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Vodacom Tanzania kwa mara ya tatu mfululizo.

Kwa sasa Simba ina alama 71 ambazo zimewaweka kileleni mwa msimamo na ikifikisha pointi 83, haitaweza kufikiwa na timu yoyote, hivyo kuifanya kutawazwa mabingwa wapya.

Aidha, Sven amesema wakifanikiwa kupata alama hizo atakuwa anafanya mabadiliko ya kikosi mara kwa mara ili kuwapa nafasi wachezaji waliokuwa hawachezi, huku wakielekeza nguvu katika michuano ya FA ambayo wamefika hatua ya robo fainali.

"Mipango ya timu ni kuhakikisha tunapata pointi 12 ili kutwaa ubingwa wa ligi mapema, halafu tunaweka nguvu kwenye michuano ya FA.

"Na kama tukifanikiwa kupata pointi hizo kuna wachezaji tutawapa nafasi kubwa ya kucheza ambao walikuwa hawapati namba mwanzoni," alisema Sven.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >